Yeye Aliye Ndani Yenu

Asante, Ndugu Neville. Bwana akubariki.

Hebu tuendelee kusimama kidogo tunapoomba. Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Na wote ambao wangetaka kukumbukwa katika maombi haya, inueni mikono yenu mseme, "Mungu, ni mimi."

2 Mungu uliye Mtakatifu sana na Mwenye Neema nyingi, tunawaleta watu hawa mbele Zako, pamoja na maombi waliyo nayo. Waliomba wakumbukwe. Na, Bwana, mkono wangu umeinuliwa pia. Nakuomba Wewe uturehemu. Wewe wazijua haja zetu, nasi tungeomba, kama vile Wewe ulivyotufundisha kuomba, "Ufalme Wako uje. Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani, kama huko Mbinguni." Baba, tunaomba rehema usiku wa leo, uhuru wa Roho, ili tuweze kuwaletea watu Kweli ya Injili, na kile tunachoamini kuwa ni Ujumbe wa wakati huu, kwa ajili ya Kanisa Lako. Bwana, tukiomba kwamba tu sehemu ya Kanisa lile ambalo litaitwa katika siku za mwisho! Baba, kama sisi si sehemu ile, basi tufunulie litupasalo kutenda ili tuwe sehemu ile. Na utupe neema, nguvu, katika saa hii ya kujaribiwa iliyopo duniani kuwajaribu hao wote wakaao hapa. Tupe Roho Wako Mtakatifu, kutuelekeza na kutuongoza, ili tuweze hatimaye, mwishoni, kuja Kwako kwa amani, kwa ule Uzima wa Milele ambao waamini wote wameutazamia tangu mwanzo wa wakati. Tusaidie, Bwana. Twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

3 Kwa kweli nina furaha kwa majaliwa ya kuwepo huku usiku wa leo—usiku wa leo, na kwa neema ya Mungu tuliyopewa katika Yesu.

4 Na halafu kuhusu ule—ule Ujumbe asubuhi hii, sasa, nataka kila mmoja aelewe kinaganaga. Sasa, natumainia kwa Mungu kwamba wakati huo haujawadia. Unaona? Lakini huo Ujumbe ni wa kweli. Huo Ujumbe ni wa kweli. Utatimia, utatimia wakati fulani, kama huu sio wakati huo. Na inaonekana kabisa kama ndio wakati huo, mpaka nikajisikia kama Paulo wa kale, aliyesema, "Sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote," unaona, kila kitu kinachopaswa kutendwa.

5 Kulikuwa na jambo moja ambalo nilitenda asubuhi hii, ambalo ninasikitika nimelitamka. Ni—nilitaja jina la ndugu fulani ambaye nadhani yuko makosani. Sikupaswa kufanya hivyo. Sitaji kamwe jina la mtu; na ikitokea kwamba ataipata hiyo kanda. Nami nataka kumwona na kuzungumza naye, kwa sababu nafikiria ndugu huyo, mtu maarufu, mtu mzuri ambaye amehubiri papa hapa kwenye mimbara hii, Ndugu David duPlessis. Nami sikukusudia kulitaja jina lake. Nilishikwa na

hofu juu ya Ujumbe, na kadhalika, kuhusu vipi kama wakati umewadia, nami nikalitaja jina la yule ndugu. Sitendi jambo hilo. Ninasikitika nililitenda hilo. Ninampenda Ndugu David duPlessis. Yeye ni ndugu yetu, nami—nami nafikiria kwamba mtu hodari jinsi hiyo angepaswa kuwa na ujuzi zaidi wa Maandiko.

Nitawaambia ni nini. Ni, mazungumzo ambayo tulikuwa nayo mimi na David . . .

6 Wakati fulani alizungumza kwa niaba yangu mikutanoni. Alihubiri papa hapa kwenye mimbara hii, au kanisa la kale, hapa toka kwenye mimbara. Na ndugu yake, Justus, alikuwa mkalimani wangu huko Afrika ya Kusini, ambako ninarejea. Nao wanatoka kwenye jamaa nzuri, nyumba ya Kipentekoste, mtu mzuri hasa. David alikuwa, ninaamini, mwenye kiti, wakati mmoja, wa Pentecostal Assemblies Ulimwenguni, na kwenye Baraza la Wapentekoste Ulimwenguni. Alikuwa mmoja wa wenye viti. Na baadaye akaja Marekani akahamia huku, huko Texas, pamoja na Ndugu Gordon Lindsay, halafu akaanza kuhubiri sehemu mbalimbali.

7 Lakini jambo ni kwamba, mahali ambapo ninafikiria kwamba ndugu yetu wa thamani alikosea; kama tu niwezavyo nami kukosea, au mtu mwingine ye yote; alianza kujishughulisha na mambo ya hali ya juu. Alishikilia kuzungumzia kuhusu Chuo Kikuu cha Princeton na sehemu ambazo zilikuwa zinamwalika yeye, akifikiria kwamba alikuwa akitenda yaliyo sahihi, na alikuwa akitia chakula cha mifugo moja kwa moja kwenye mashine; unaona, na shangwe kubwa sana!

Na si hilo tu, bali Wafanyi Biashara wa Injili Yote, ambao huidhamini mikutano yangu, ulimwenguni kote—kote. Unaona? Na—nawapenda watu hao, unaona, lakini kwa kweli sikubaliani nao juu ya kanuni ambazo wao—wao wana—wao wana . . . Wame—wameondoka toka ambapo, kanuni zao, walipoanza, na sasa wanakuwa kama tu madhehebu mengine yo yote au cho chote kile. Unaona? Na jambo ni kwamba, wao hawajaribu kudumu wapentekoste, lakini wanajaribu kuchanganya pentekoste na mengine yote pamoja.

8 Na inaonekana kwangu kama kwamba Ndugu duPlessis, mtu mzuri sana na stadi kama huyo, angejua vya kutosha kuhusu Maandiko hata wakati aonapo yule mwanamwali mpumbavu akijaribu kununua Mafuta, wakati umepita. Unaona? Kumbuka, wakati alipokuja kununua Mafuta, Mafuta yalikuwa yamekwisha kabisa. Hayo ni Maandiko. Naye akasema, "Tupeni Mafuta yenu," kwa Kanisa, [Ndugu Branham anagonga mara nne mimbarani—Mh.] lakini hakuyapata Hayo. Anaweza kuruka juu chini, anene kwa lugha, na cho chote kile, lakini, kulingana na Neno Lenyewe la Mungu, hakuyapata Hayo.

Naye alikuweko nje kwenye giza la nje; nako kulikuwa na kulia, kuomboleza, na kusaga meno, wakati Bibi-arusi aliyechaguliwa alipokwisha kuingia. Yule—yule mwanamwali mwenye busara alikuwa na Mafuta kwenye taa yake.

9 Sasa, na—namjua mtu mwingine, kitu fulani ambacho ndio kwanza kitukie hivi majuzi. Jambo ni kwamba, ni watu hawa wazuri, unaona, wakipata kidogo, unajua ninalomaanisha, wakipata nafasi ndogo miongoni mwa watu. Na punde si punde, wanajisikia kwamba huyo ni Mungu anayetenda jambo hilo. Na mara nyingi, huyo ni Ibilisi anayetenda hilo. Unaona?

10 Yesu alikuwa na nafasi ya kuja mbele ya Herode; Yeye alikuwa na nafasi mbele ya wengi, nao walitaka kumtumia Yeye kwa maonyesho. Unaona?

Hayo ndiyo tu wanayojaribu kufanya kwa Pentekoste. Pentekoste ilitoka kwenye mambo hayo, iwe tofauti. "Na kama nguruwe anayegaa-gaa matopeni, na mbwa kwenye matapiko yake, imerudi mle tena," na sasa imo katika Barasa la Ekumeni. Unaona? Ni vibaya sana. Ni aibu.

11 Mungu na aniweke mnyofu na mnyenyekevu, ili Yeye aweze kufunua Kweli Yake. Unaona? Sitaki kamwe kufanya hivyo; sitaki taa zenye kung'aa, na sitaki mioto na kimulimuli cha ulimwengu. Hebu nishike njia na wachache wa Bwana wanaodharauliwa. Hebu nidumu katika Neno.

12 Sasa kuzungumzia kuhusu Baraza la Ekumeni likiungana na Vatican. Je! mnaamini kwamba wangeweza kuungana katika Neno? Wangeweza katika madhehebu, bali hawawezi katika Neno. Unaona? Hiyo ni kweli. Kwa hiyo hakuna cha kupatana. Unaona? Madhehebu, yote ni sawa tu, kila kitu ni sawa; kimenyooka vizuri sana, mama na binti. Lakini ifikapo kwenye Neno hili, niko imara tu dhidi ya Methodisti na Batisti na Wapresbiteri, kama nilivyo dhidi ya Ukatoliki, sababu ni mama na binti, kulingana na Neno hili. Ninasimama na hili Neno, unaona, *Hili,* kila Neno Lake.

13 Sasa, huyu ndugu wa thamani, yeye na mkewe ni rafiki zangu wa karibu. Wengi wenu mmeona lile gazeti, jinsi ambavyo huyo ndugu wa thamani, ndugu aliyetumwa na Mungu angeweza kumwachilia mkewe . . . Mtu fulani alimwambia alionekana kama Jacqueline Kennedy, na alikata nywele zake kubwa kwa mtindo wa kisasa na kadhalika. Ni nini? Anashirikiana na watu wa namna hiyo, wakati wote, na hatimaye . . .

Mtu mzuri akimchukua mwanamke mbaya, huyo mwanamke huenda atakuwa mwanamke mzuri ama . . . Ninamaanisha, mwanamume mzuri akimchukua mwanamke mbaya, aidha huyu mwanamke atakuwa mwanamke mzuri ama yeye atakuwa mwanamume mbaya. Nionyeshe mwenzako, nitakuambia wewe ni nani. Unaona? Watu wa tabia moja, huambatana. Usikaribie vitu vinavyometameta!

14 Nilishuka chini kwenye migodi, juzijuzi, huko juu sana kwenye milima ya Arizona na—na mpaka wa Mexico. Mimi na Ndugu Sothmann, anayeketi hapa, tulikuwa juu kule pamoja. Nami niliingia ndani mle na kuchimba fungu la . . . Inafanana kabisa na dhahabu. Lakini njia pekee unaweza kujua si dhahabu, inametameta zaidi ya dhahabu. Inametameta. Na dhahabu haimetameti, inameka. Unaona? Na jina lake, ni "dhahabu ya mjinga." Hata haina thamani kama ya mwamba inamokaa. Inaitwa mrututu wa chuma. Nadhani, kwenye ile—ile . . . Wanasayansi hudai kwamba maji na asidi zinazovuja, na kadhalika, hayakuingia hapo vya kutosha kuifanya ngumu na kuifikisha mahali pa kufanyika dhahabu. Kwa hiyo—hiyo humetameta vizuri zaidi, lakini haina ile kemikali ndani yake.

Na hivyo ndivyo ulivyo Ukristo mwingi wa kujifanya kuamini, unaona, utametameta, na kama ilivyo Hollywood. Lakini Kanisa linameka kwa Injili. Unaona?

15 Sasa, dada fulani hapa, ndio kwanza Billy anionyeshe, alikuwa mwema vya kutosha kuchukua gazeti hili la *Life,* picha hii, na kuikuza, ya wale Malaika saba, na akaipiga picha akanitumia. Picha hiyo ndiyo ile. Na sasa kama utaangalia hapa, wakati walipokuwa wanaondoka, wakipaa kurejea, Malaika walipokwisha kuleta Ujumbe wao, lilikuwa katika umbo la piramidi; sawa kabisa na nilivyowaambia, miezi mitatu kabla ya jambo hilo kutokea, jinsi ingekuwa. Hilo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Na yule Malaika aliyejitokeza sana, huku mabawa yake yako ubavuni, nyuma, yamewekwa nyuma, mnamkumbuka Yeye. Kasema, "Kichwa Chake . . . akija kasi hivi." Hata huoni mabawa *pale*? Yule Malaika *pale,* kulingana kabisa na vile lilivyosemwa.

16 Sasa, ni Mungu tu awezaye kutenda jambo hilo. Wana picha iliyopo hapa, pia, ya mwanamke ambaye alisema . . . Mara nyingi, watu husema . . .

17 Katika u—upambanuzi, husema, "Mtu huyu ana kivuli cha mauti, kivuli cheusi."

18 Sasa wanasema, "Naam, ni kusema tu anasema hivyo." Unaona, hao ndio watu ambao hawawezi kwenda umbali wote, hawawezi kuona jambo hilo. Wanaweza kupaza sauti pamoja nawe, wanaweza—wanaweza kuzungumza nawe; lakini inapofikia kuamini yote hasa, nafsi yote na mwili wote, hawawezi kufanya hivyo.

Kwa hiyo, lakini unaona, kama Mungu yu katika jambo hilo, na kusema Kweli, huu ni wakati wa mwisho wa historia. Hii ndiyo historia ya mwisho ya ulimwengu. Unakwisha. Hakutakuwa na wakati tena, siku moja. Mungu anathibitisha kila kitu, vyote viwili kiroho na kisayansi.

19 Niliposema, nikiwa mvulana mdogo, "Nguzo ya Moto, ilifanana na nyota."

20 Wangapi wanakumbuka, hapo kale, walizoea kuiita Hiyo "Nyota"? Yeye alipotokea chini hapa mtoni, wakati Yeye aliposema, "Kama Yohana Mbatizaji, alivyopelekwa . . . "

21 Sasa, hatimaye, Hiyo ikashuka, na ile picha Yake ikapigwa. Tulikuwa na moja hapa, mahali fulani. Ndiyo, wanasema iko pembeni kule; siwezi kuiona. Kisayansi inathibitisha hiyo ni Kweli.

22 Na sasa, kusema watu "wana kivuli." Sasa, alikuwapo mwanamke, picha. Ndiyo hiyo hapo, kawaida, kama picha nyingine yo yote; kama mtu anayepiga hii, mtambo. Nikasema . . . Mtu fulani alikuwa anashangaa kuhusu hiyo. Naye akamwambia yule mwanamke, "Una kivuli cha mauti, cha kansa. Kuna kivuli cheusi juu yake." Akageuka akapiga picha. Yule mwanamke amekuwa hapa kushuhudia, na pengine yupo hapa usiku wa leo, nijuavyo mimi. Unaona?

Naam, *yule* pale mwanamke aliye na kitu kama shela nyeusi juu yake. Sawa, sasa, huo pale uthibitisho wa kisayansi kwamba hilo ni kweli. Na mara baada ya yule mwanamke kutangazwa yu "mzima," wakapiga picha, na hakikuwepo. Nini kilipiga lenzi wakati huo? Na nini kimeondoka, ambacho haki—hakikuwa kwenye lenzi wakati yeye alitangazwa kwamba ameponywa? Unaona?

Sasa, nikisimama hapa, niliwaambia kwamba wale Malaika a wanakuja.

23 Ndugu Fred, akiwa mmoja . . . Nilimwona ndugu Fred muda mchache uliopita. Nilidhani alikuwepo papa hapa, lakini nimemkosa mahali fulani. Loo, nyuma hapa, sawa. Alikuwa amesimama kwenye—maili mbili, au maili moja na nusu, au mbili, kutoka pale nilipokuwa; alisikia mlipuko, akasikia ule mtikiso na kila kitu kingine, wakati ulipolipuka. Hiyo ni kweli, Ndugu Fred?

Na hapo walikuwepo Malaika waliotumwa na Ujumbe. Na hata ipo hapa katika umbo la piramidi, kama nilivyowaonyesha jinsi ingekuwa hapa, nilivyowaambia jinsi wangekuwa wamesimama, kabla sijaondoka.

Picha baada ya picha, kote nchini, walilipiga, hadi Mexico, likiwa maili thelathini kwenda juu na maili ishirini na saba kukingama. Na liko juu sana hata unyevu au kitu cho chote chaweza . . . Unyevu hausafiri juu zaidi ya maili kama nane au tisa, kwenda juu, halafu walikuweko nje mahali ambapo hakuna kitu cha kufanya unyevu. Unaona? Na hili lilikuwa, nadhani lilikuwa ama maili ishirini na saba kwenda juu na maili thelathini kukingama, au ama ilikuwa—ilikuwa ishirini . . . au maili thelathini kwenda juu na maili ishirini na saba kukingama, mojawapo. Gazeti la *Life* lilikinakiri, au la *Look*. Lilikuwa ni lipi, *Look* au *Life*? *Life,* gazeti la *Life*. Nafikiri, toleo la Mei 17. Sawa.

24 Sasa hilo hapo, kisayansi, uthibitisho kwamba ni Kweli, kwa hiyo basi sisi—sisi hatuna wasiwasi kama ni Kweli; yote mawili kisayansi, na kiroho, na yaliyonenwa yalitimia. Kwa hiyo, Ujumbe wa zile Muhuri Saba, zinapomalizika, huo ndio Ujumbe wa Biblia nzima. Zile Muhuri Saba zinamaliza Agano Jipya na kuitia muhuri. Hiyo ni kweli. Sasa, tunajua kwamba ndivyo ilivyo, kwa usemi wa kinabii, kwa kisayansi, na kwa Neno. Vitu vitatu vimeshuhudia jambo hilo, kwamba ni Kweli.

25 Kwa hiyo, tunajua kwamba tuko katika wakati wa mwisho. Tumefika. Sijui ni umbali gani, mimi—mimi . . . Yeye kamwe hataturuhusu kujua jambo hilo, kwa sababu Kuja Kwake kutakuwa "kama mwizi wakati wa usiku." Rafiki zangu, ndugu yangu, dada, hebu na tuwe tayari, haidhuru. Hebu na tujitakase. Unaona? Kwa sababu, ulimwengu utaendelea mbele tu. Hata hawatajua kamwe limetukia. Wakati milango ya rehema itakapofungwa, wahubiri watakuwa wakihubiri wokovu, wata—watakuwa wakiwafanya watu kutubu, wakiendelea kama tu ilivyokuwa sikuzote. Ilitendeka katika nyakati zingine, na ilitendeka katika . . . Itatendeka katika wakati huu.

Na Kunyakuliwa kutatokea ghafla sana na haraka sana, hata ulimwengu hautawakosa, kwamba wamekwenda. Hiyo ni kweli. Hawatajua kitu juu yake. Yeye anakuja kumnyakua kisiri. Litakuwa limekwenda, nao hawatajua kitu juu yake.

Kwa hiyo, dumuni katika maombi. Niombeeni. Nitawaombea. Hatujui saa hiyo itakuwa ni lini, lakini tunaamini itakuwa hivi karibuni. Kaeni mbali na vitu vinavyometameta. Dumuni katika Injili, unaona, kaa papo hapo sasa, na uombe.

26 Sasa, Billy aliniandikia barua hapa, au kijikaratasi hasa, akasema mtu fulani alitaka kumweka mtoto wakfu. Kama hiyo ni kweli, (sivyo?) inua mkono wako juu, ikiwa baadhi . . . Ndiyo, watoto wawili. Sawa, waleteni moja kwa moja. Na Ndugu Neville . . . Basi sijui iwapo dada yetu kwenye piano atakuja hapa kwa muda kidogo, kwa ajili ya kuweka mtoto wakfu. Hatutaki kumwacha ye yote.

27 Sasa, kumbuka, mnamo wakati kama huu kesho usiku, Bwana akipenda, nitakuwepo katika Jiji la New York. Nasi tunakwenda huko kwenye uwanja wa vita, "kupiga vita vile vizuri vya Imani."

28 Kwa hiyo papa hapa, dada, tafadhali. Papa hapa mbele, nami nitavichukua. Ndiyo, mama. Asante. Na sasa tuna . . .

29 Wangapi wataniombea? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, kama Mungu akipenda; ambalo, natumaini Yeye anapenda; Jumapili, ya juma lijalo . . . Kama ni sawa kwa Ndugu Neville. [Ndugu Neville anasema, "Sawa."] Jumapili, ya juma lijalo, nitarejea tena, nikiwa njiani kwenda zangu Louisiana, na kusimama kidogo kwa ajili ya mkutano hapa kanisani. ["Amina."]

30 Nataka kuwashukuru ninyi nyote kwa fadhili zenu. Bibi yule aliyenipelekea peremende zile juu kule, na—nafurahia hilo. Sijui huyo bibi alikuwa ni nani. Mtu fulani alinipelekea kasha la peremende na viyoga namna hiyo. Kwa kweli ilikuwa, tamu sana. Nimeshiba hiyo sasa hivi, na na—nawashukuru. Na unafikiria hayo mambo madogo hayamaanishi kitu? Hakika yanamaanisha; zawadi ndogo. Na watu mbalimbali wakileta zawadi zao za upendo. Na kumwonyesha Billy Paul, na kuzitoa, na kadhalika. Ni—ninazipokea, unaona. Hujui jinsi ninavyozifurahia! Mungu awabariki. Nitazikumbuka, unaona, je! jinsi gani zaidi Yeye huzikumbuka hizo. "Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, mmenitendea Mimi." Unaona? Sasa, Rehema itaonyeshwa wakati rehema inapotolewa.

31 Sasa, tuna watoto wadogo wazuri hapa. Unge… Nawatakeni mkae pale na muimbe *Waleteni*, baadaye. Sawa, ninyi ndugu njoni juu huku kidogo.

Jamani, huyu hapa wa kwanza, jozi ndogo ya macho ya hudhurungi yanayoniangalia, na tabasamu kubwa, nzuri. Msichana mdogo, anaitwa…[Mama anasema, "Sharon Rose. Sharon Rose."] Sharon Rose, hilo ni jina maarufu kwangu. ["Tulimpa jina, Ndugu Branham, kwa jina la wako."] Kwa jina la msichana wangu ambaye amefariki. ["Tulimpa jina hata kabla ya kuzaliwa, Ndugu Branham."] Walimpa jina kabla ya kuzaliwa. Kama angekuwa msichana mdogo, mngemwita Sharon Rose. ["Tulikuwa na hakika atakuwa msichana. Yeye, ilibidi awe."] Ilibidi awe. ["Sharon Rose Goodman."]

Mnajua nini? Sijui kama mnajua au la; kama mke wangu alikuwa amesimama hapa, labda angezimia. Nguo hii ni kama ile ambayo msichana wangu mdogo alikuwa amevaa wakati wa kuwekwa wakfu, mtoto Sharon Rose. Huyu aweza awe…Huyu na aishi; ambapo, Mungu alimchukua wangu.

Jina lako la mwisho ni nani? [Yule mama anasema, "Goodman."] Bibi na…Unatoka hapa mjini? ["Chicago."] Chicago. Ndugu na Dada Goodman, Mungu awabariki.

Basi, unajua, Sharon wangu mchanga alifanana na huyo. Sidhani kuna ye yote hapa anayemkumbuka jinsi alivyokuwa. Alikuwa na macho madogo ya hudhurungi kama hayo, kama mama yake, msichana mdogo anayependeza sana mwenye nywele nyeusi. Kama tu…

Mtoto huyo ana umri gani? [Mama anasema, "Miezi mitano."—Mh.] Miezi mitano. Yeye alikuwa na miezi minane Mungu alipomwita kule juu. Nilimwona, kwa muda mfupi baadaye. Mnaijua hadithi hiyo. ["Tunayo huko nyumbani, kwenye kanda."] Mnayo nyumbani, katika kanda.

Sharon Rose linatoka katika Neno. Nililigeuza, kutoka, "Rose of Sharon." Naye alihitaji mmoja mdogo, mmoja wao,

kwenye madhabahu Yake, kwa hiyo Yeye akamchukua. Unaona? Nami nitakuwa pamoja naye tena. Sharon wenu mdogo na ajaliwe kuishi apate kutimiza maisha yale ambayo huyo angeishi hapa duniani. Na awe pamoja nanyi Utukufuni, kama ninavyojisikia Sharon wangu atakuwa pamoja nami.

Washindaje? Unaona? Wanena kuhusu kitoto kidogo kipendezacho, mwangalie huyu! Amejaa tabasamu tu.

Tuinamishe vichwa vyetu.

Mungu mpendwa, ninaposhikilia hazina hii ndogo, kitoto Sharon Rose. Unajua moyoni mwangu, Bwana, ninalowazia, kwa hiyo sina haja ya kulielezea. Bwana Mungu na abarikiwe atupaye vito hivi vidogo mioyoni mwetu! Ibariki nyumba hii ya Goodman. Jalia wazazi waheshimiwe, nao wanaheshimiwa, kuwa na kito kama hiki nyumbani. Jalia kikae nyumbani mwao, Bwana. Na kama kuna kesho, mfanye mwanamke mwenye heshima kwa ajili ya kesho.

Na sasa, Bwana Mungu, kwa kutii ambalo Wewe ulituagiza, kwa mfano Wako, kutenda, Wewe uliwachukua watoto wachanga mikononi Mwako na ukawabariki, ukasema, "Waacheni watoto wadogo waje Kwangu." Nao wanamleta mtoto kwangu, nikiwa mtumishi Wako, kama Wewe ulivyosema watumishi Wako waiendeleze kazi Yako. Na hapa wanasimama watumishi Wako, Ndugu Neville, Ndugu Capps, na mimi mwenyewe. Na sasa, Bwana Mungu, toka kwenye mikono ya baba na mama, tunakupa Wewe kitoto Sharon Rose Goodman, ambaye tunamweka wakfu kwa ajili ya maisha ya utumishi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu akubariki. [Dada Goodman anasema, "Ndugu Branham, pia tunao watano zaidi nyumbani, wasichana wawili na wavulana wawili,"—Mh.] Watoto wadogo watano, licha ya huyu. ["Ndiyo."] Jinsi linavyopendeza! Mungu akubariki, Ndugu Goodman. Mungu akubariki, Dada Goodman. Na Bwana na ambariki mtoto Sharon!

U hali gani ndugu? Sasa hebu tuone, mimi—mimi... Arnett. [Baba anasema, "Arnett."—Mh.] Arnett. Arnett, sawa. ["Ameitwa kwa—kwa jina lako."] Hilo ni sawa? William, William Arnett? ["James William Arnett."] James William Arnett. Huyo ni mvulana mzuri. Unajua, tuna baadhi ya mambo tunayoshirikiana, yeye na mimi, tayari; majina, na halafu tunachanua nywele zetu sawa, unaona. Yeye ni mvulana mzuri. Jimmy. Nadhani ndivyo mnavyomwita, James? ["James."] James, basi, sawa.

Sijui kama ningeweza kumshika? ["Anaweza akakuruhusu."] Sijui. Sasa, Jimmy, vema, tu marafiki kweli. Unajua hivyo, siyo? Sawa.

Tuinamishe vichwa vyetu.

Bwana Mungu, Wewe umeibariki nyumba hii, nyumba ya Arnett walio pamoja na mvulana huyu mdogo na mzuri. Basi naomba kwamba Wewe utambariki baba yake, mama yake, wapenzi wake. Wao ni Wakristo. Jinsi ambavyo baba yake amepiga vita sana, hizo sigara na vitu mbalimbali, kutoka... Siku moja ikatokea, "BWANA ASEMA HIVI." Yeye alikuwa kama yule mwanamke aliyeng'ang'ania kwamba atafika pale. Ingawa biashara yake iliharibika, na kila kitu kilionekana kuwa kinaharibika, bado alichukua sehemu ya fedha zake naye akangojea mahojiano baada ya mahojiano, hata asubuhi moja ikatukia. Yeye aliamini kwamba ingetukia.

Sasa yeye anamleta mvulana huyu mdogo ambaye Wewe umembariki kwake, Ee Mungu, tunda la muungano wao. Nambariki huyu mtoto James William Arnett, katika Jina Lake Yesu Kristo. Mpe maisha marefu. Mfanye mtu anayeistahili Injili Yako kwa ajili ya kesho, kama kuna kesho. Na, hatimaye, katika Ufalme ujao, na tuwe kule pamoja. Mimi kama watumishi Wako, tunaweka mikono yetu juu yake na kumweka wakfu kwa Yesu Kristo, kwa maisha haya ya utumishi. Amina.

Ubarikiwe. Mungu akubariki, ndugu. Nina wawili zaidi? Hawa ndio wale wale. Sawa.

Ninaamini karibu ungeweza kunibeba, badala ya mimi kukubeba wewe. Na huyu ni...[Ndugu Arnett anasema, "...?..."—Mh.] Alfred, na Al na Martha. Hebu acha kusanyiko, nataka wawaone watoto. Nadhani, wanapokuwa wadogo, wachanga, wanapendeza.

Sasa hebu tuweke mikono yetu juu yao.

Na vile vile, Mwenyezi Mungu, sisi watumishi Wako, twaweka mikono yetu juu ya watoto hawa, ndugu mdogo na dada wa mvulana huyu mdogo ambaye ndiyo tu tumemweka wakfu hapa. Tunaweka mikono yetu juu yao kwa ku—kuwaweka wakfu, toka kwa mama na baba, kwenye mikono ya Yesu Kristo, kwa maisha ya utumishi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu awabariki. Al na Martha, dada, inapendeza sana kuwaona tena. Bwana awe nanyi.

Kijana huyu mdogo, jamani, ni mvulana mzuri. Nilikuwa naweza kugawanya nywele zangu namna hiyo. Unaona? Jina lake ni nani? [Babaye anasema, "Terrell Keith Walker."—Mh.] Ke-...["Terrel Keith Walker."] Herrel Keith Walker. Mvulana mzuri jinsi gani!

Nashangaa, sijui, mnaona. Ananitazama kana kwamba angeweza. Sijui kama naweza kumshika? [Yule mtoto ananena—Mh.] Sivyo, Keith? Loo, ni mvulana mzuri. Bila shaka. Huyo si mvulana anayependeza? Harrell. [Mamake anasema, "Terrell."] Terrell, Terrell Keith Walker.

Mwenyezi Mungu, toka kwenye mikono ya wazazi hadi kwenye mikono ya Yesu Kristo, mtoto Terrell Keith Walker, twaweka mikono yetu juu yake kwa kumweka wakfu kwa Mwenyezi Mungu. Kama baba na mama wanavyotamani sana kwamba mtoto huyu atalelewa katika maonyo ya Mungu. Kama kuna kesho, mfanye mtumishi anayestahili huku kuwekwa wakfu, kwani sisi watumishi Wako tunaweka mikono yetu juu ya mtoto huyu mchanga na kumtoa kwa Bwana Yesu Kristo. Amina.

Ubarikiwe, Ndugu Walker. Huyu ni Dada Walker? [Dada Walker anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] Ni vizuri sana. Una mvulana mzuri, na Mungu awabariki.

[Ndugu Gramby anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Sawa, bwana. [Ndugu Gramby anaendelea kuzungumza.] Ndiyo. ["Na kumwombea alipozaliwa. Alizaliwa na fundo kwenye taya lake. Nawe ulimwombea, na hiyo iliondoka mara moja."] Msichana huyu mdogo, ni Ndugu Grimsley wetu . . . [Yule ndugu anasema, "Gramby."] Gramby. Ni—ninachanganya hilo. Nina Ndugu Grimsley, ninashikilia kufikiria . . . Ndugu Gramby anamleta msichana huyu mdogo. Na wakati alipozaliwa, alikuwa na fundo kubwa kwenye uso wake. Nami nilimwombea, na hilo fundo likaondoka. Na sasa wanataka kuomba, kwa sababu . . . Wazazi ni Wakristo? ["Sio Wakristo."] Sio Wakristo. Nao wanahofu kwamba pepo mchafu anataka kumtwaa mtoto huyu, nao wanataka aondolewe.

Hebu tuombe.

Bwana Yesu, juu ya mtoto huyu mdogo, anapoegemea madhabahuni . . . Ambapo, Wewe umeonyesha neema, kuondoa uvimbe wa fundo kinywani mwake. Sasa pepo mchafu anajaribu kuyaangamiza maisha ya mtoto huyu. Bila shaka Wewe ungeweza kumtumia msichana huyu mdogo, na unapanga kufanya hivyo, na Shetani anajaribu kuvuruga mpango huo. Kwa hiyo, tunamwamuru Shetani, katika Jina la Yesu Kristo, kuondoa mi—mikono yake na yeye mwenyewe toka kwa mtoto huyu; tunapomtoa kwa Bwana Yesu Kristo, kwa utukufu wa Mungu. Amina.

Ndugu Gramby, amini. Mtoto ni mdogo sana hata ni vigumu awe na imani, lakini itakuwa hivyo.

32 Nampenda Yeye. Nanyi je? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye ni wa ajabu.

Sasa, kila mmoja, niliahidi usiku wa leo kwamba ningemaliza mnamo saa mbili na nusu, kwa hiyo hiyo inanipa nusu saa. Sijui sasa kuhusu jambo hilo. Naweza tu niwe nimechelewa kidogo zaidi. Lakini hebu sasa sisi . . .

33 Ninafurahi kumwona Ndugu Dauch hapa asubuhi hii. Na sijui wapi mtu yule mwingine alikokwenda; bali asubuhi hii, kama aliwahi kuwa na mtu aliyefanana naye, kulikuweko na

mtu aliyekuwa ameketi papo hapo nyuma kule, alifanana naye kabisa. Nilisema, "Ndugu Dauch ni yupi?" Nikatazama huku na huko, nami nilikuwa karibu kuliita; nami nilikuwa nimeingia sana katika Ujumbe. Unajua, Ndugu Dauch, unaonekana kama tu ulivyokuwa unaonekana sikuzote. Ninafurahi sana kumwona katika hali hiyo.

34 Hivi karibuni, nilipata simu ya mbali toka Tucson, kumwombea tena, kwamba amepatwa na jambo lingine. Ndugu Dauch ana, nadhani, umri wa miaka tisini au tisini na mmoja. Ana umri wa miaka tisini, naamini, au tisini na mmoja. Na mwili wako unadhoofika. Lakini, "Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu humponya hayo yote." Na wakati mwingine, wakati mwili unapofikia mahali ambapo hauwezi kustahimili tena, najua yeye anashikilia kwenye Mkono. Hata uwe ni donge la vumbi, Mungu aliahidi kuufufua tena, siku za mwisho. Nami ninashukuru sana.

35 Nakumbuka Ndugu Dauch, alipokuja kwenye kidimbwi hapa kubatizwa katika Jina la Bwana Yesu Kristo, naye hata hakuwa na nguo zo zote hapa za kubatizwa, lakini alitaka kwenda kwa vyo vyote. Na Mungu amemrehemu mtu yule. Hebu fikiria, ana miaka ishirini zaidi ya wakati ule ambao Mungu alimwahidi. Unaona? Kama hiyo siyo neema!

Na alikuwa mahututi, juzijuzi, akiwa na ugonjwa wa moyo kukoma kupiga kabisa, na, isitoshe, ugonjwa mbaya wa moyo, unaona. Na kama Mungu hakumponya mtu yule na kumwinua toka hapo, mara moja. Nami naamini, tangu wakati huo, tabibu wake amefariki. Hilo ni kweli? Ninael. . . Ndiyo, kwamba hata yule tabibu, tabibu wa Kiyahudi ambaye—ambaye alikuwa anamtibu, na kadhalika, na akasimama kwenye ukumbi ule na kunizungumzia mimi kumhusu yeye, amekwisha kuaga dunia. Unaona?

Jamani, kiasi gani, jinsi ulivyo na kina upendo Wako, Ee Bwana! Jinsi upendo Wako ulivyo mkuu!

36 Sasa, tuna vitambaa hapa ambavyo tutaviombea, hivi punde. Lakini nitawazungumzieni kidogo juu ya imani, halafu tutaona jinsi Bwana atatuongoza, tutakayofanya baadaye. Vema, hebu na tumwachie Yeye jambo hilo, hiyo ndiyo njia bora zaidi ya yote. Loo, kuketi pamoja katika ulimwengu wa roho!

37 Nilizungumza na baadhi ya rafiki zangu, leo, baada ya kutoka Blue Boar kule. Nami nikasema, "Mtangojea ibada?"

38 "Ndiyo."

39 Nikasema, "Pengine itawalazimu kusafiri kwa gari mpaka saa sita au saa saba." Wanatarajia kufika nyumbani mnamo saa kumi na mbili asubuhi, ni mbali mno. Kumbuka, wao ni binadamu, na huchoka kama vile mimi. Chini huko Tennessee, na vitongoji vyake, wanakwenda. Bwana awabariki.

40 Kuna mambo mengi sana ningeweza kusema; ninachukua tu muda wote. Lakini mimi—sipati kuwaona mara nyingi, mimi—mimi—napenda kuzungumza nanyi, kwa vyo vyote. Lakini kama sipati kuwaambia yote ninayowawazia ninyi, hapa, . . . Unaona?

Nataka kuwaambia hao ndugu. Baadhi yao walifunga makanisa yao.

41 Ndugu Jackson, hapa asubuhi hii, alitoa tafsiri ile nzuri sana ya—ya lugha isiyojulikana ambayo ndugu fulani alinena kwayo, na akithibitisha au akiunga mkono kwamba Huyo alikuwa ni Mungu. Uliona, Yeye hakusema kamwe Hilo lilikuwa makosa, Yeye kamwe hakusema Hilo halikuwa hivyo; Yeye alitoa ilani kusikiliza. Unaona? Unaona? Kwa hiyo, Ndugu Junior alikuwepo hapa asubuhi hii, naye alilifunga kanisa lake.

Nami nasikia ndugu wengine toka kule chini . . . yale makanisa mengine, kutoka hapa Sellersburg.

42 Na—na Ndugu Ruddell, alikuwepo hapa asubuhi hii. Sijui kama wapo hapa usiku wa leo au la. Sawa, hapa tena usiku wa leo! Vema, Bwana akubariki, Ndugu Ruddell. Na wewe . . .

Siwezi tu kulielezea, lile tu ninalofikiria. Lakini labda . . . Vema, tutakapofika upande ule mwingine, nataka niketi nanyi kwa kama miaka kumi elfu, kila mmoja wenu, unaona. Halafu, unaona, tutayazungumza yote tena.

43 Na wakati mavuno yameiva, na watenda kazi ni wachache, hebu na tuingie ndani yake, kwa bahati yawezekana kuwepo na mwenye dhambi aketiye hapa. Yawezekana kuwe na mtu fulani ambaye usiku wa leo angeweza kubadilisha mwelekeo wote.

Na kama usingekuwa wakati, asubuhi hii, usiku wa leo Vitabu vingefungwa. Kumbuka, hakutakuwa na mmoja zaidi atakayeingia wakati hayo majina yatakapokombolewa.

Kabla, sasa, kila mmoja asikilize kwa makini sana kabla ya kusoma Maandiko.

44 Wote ambao wangekombolewa, Mungu aliweka majina yao kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya ulimwengu kuumbwa. Ni wangapi wanajua hivyo? Hayo ni Maandiko. Na mpinga Kristo, katika siku za mwisho, atafanana sana na kitu halisi, Kanisa la kweli, kwa kila hali kama Yuda alivyokuwa, hata angewadanganya walio Wateule kama yamkini. Hiyo ni kweli? Lakini hakuna mtu awezaye kuja kwa Yesu isipokuwa Mungu ampeleke, na wote ambao Mungu alimpa Yeye watamjia Yeye. Naye atakapokichukua kile Kitabu, jina la mwisho.

45 Unaona, wote katika wakati wa Luther, Yeye aliwatoa. Wote katika wakati wa Wesley, Yeye aliwatoa. Wote katika nyakati mbalimbali, na wakati wa Upentekoste, Yeye aliwatoa. Wako upande huu, hawatahukumiwa pamoja nao. Watanyakuliwa. Na basi wakati jina la mwisho litakapotokea, ambalo liliwekwa

kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, ambaye alichinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu; wakati jina la mwisho limekwisha kukombolewa, kazi Yake imekwisha. Yeye anajitokeza kuja kudai ambacho Yeye amekikomboa. Hilo hufanya mioyo yetu ione huruma nyingi. Lakini kama ingeendelea miaka elfu moja baadaye, kusingekuwepo na mmoja atakayekombolewa.

Na hakuna mtu anayeweza kukombolewa isipokuwa waliandikwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Ni akina nani? Sijui. Hakuna mwingine ye yote ajuaye, unaona, ni Mungu peke yake. Natumaini kwamba kila mmoja wetu, majina yetu yalikuwa kwenye Kitabu kile. Kama langu lilikuwepo mle, nina hakika nitakuwa kule; kama halikuwepo, sitakuwepo kule. Ni hayo tu. Unaona, tu, hiyo ni kazi ya Mungu tu. "Si katika uwezo wake yeye atakaye, wala wa yeye apigaye mbio, bali Mungu arehemuye." Unaona?

46 Sasa hebu tulikaribie Neno, kwa kicho chote na unyofu. Nami nafikiri hilo ndilo jambo moja litupasalo kufanya, unaona. Hebu na tuache upuzi mwingi namna hiyo! Tuwe wenye kicho, wanyofu!

Ninaangalia maungamo yale wakati mwingine wakati wao. . .Kwenye televisheni, walipokuwa na mkutano ule wa Billy Graham; si ati nina neno dhidi ya Billy Graham. Bali kule California, mtu huyo alihubiri ujumbe mzuri sana usiku huo uliotangulia, akahubiri jambo lile lile nililohubiri hapa sio muda mrefu uliopita, juu ya Danieli, "Umepimwa katika mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka." Wangapi waliiona? Wengi wenu, nadhani.

47 Tazama, uliwachunguza wale watu wakitoka kwenye marefu ya kanisa, wakitafuna peremende, wakicheka, wakipigana makonde? Huko sio kutembea kati ya kifo na Uzima. Huko sio kusikitika kwa ajili ya dhambi, na toba. Unaona? Ni kile tu Billy alisema, "Kukata shauri." Na uamuzi, baridi, wa macho makavu, si kitu, ni bure. Yakubidi uisikitikie dhambi, na uipe kisogo.

Na Billy mwenyewe alisema, "Anathibitisha kwamba, katika thelathini elfu, huwezi kupata thelathini katika mwaka." Alisema juzijuzi, "Hivi New York ina nini? Nilikuwa na mkutano mkuu pale, na kitu gani kimetukia? Dhambi ni mbaya zaidi kuliko ilivyowahi kuwa."

48 Na itaendelea kuwa mbaya zaidi. Hakutakuwa na to. . . toba ya kitaifa. Taifa hili limekwisha. Ni ninyi tu, watu binafsi, na hivi karibuni hilo litaisha, kama halijaisha tayari. Sasa, hebu andikeni jambo hilo, ninyi watoto wadogo. Mtaona ni umbali gani Ndugu Branham. . .Si Ndugu Branham. Hilo ambalo nimesema ni sahihi au kosa. Dhambi itazidi kuwa mbaya mpaka siku moja mbingu zitashika moto, utaiangukia dunia, na

dunia itateketezwa kwa moto mkali. Lakini, waliokombolewa hawatakuwepo hapa wakati huo, watakuwa wamekwenda.

49 Sasa katika Kitabu cha Marko Mtakatifu sura ya 11, Yohana wa Kwanza 4:4 na Mathayo 28:20, nataka kusoma.

50 Sasa, kwanza, nataka kusoma kutoka Marko Mtakatifu, sura ya 11, na aya ya 12 hadi ya 24.

Sikilizeni kwa makini sana sasa tunaposoma. Na sasa hili litaunga mkono ushuhuda mdogo, na maneno machache ya kuwatia moyo, halafu tutaona ambacho Bwana atatutaka tutende. Kila mmoja aendelee kuketi na muwe katika maombi sasa, tunaposoma.

51 Marko 11:12.

> *Hata asubuhi yake walipo*. . . kuja toka *Bethania aliona njaa.*
>
> *Akaona kwa* mbali *mtini wenye majani, akaenda* kwa furaha *ili labda aone kitu juu yake; na* alipoufikia *hakuona kitu ila majani; maana si wakati wa tini.*
>
> *Akajibu, akauambia* tangu leo *hata milele mtu asile matunda kutoka kwako. Wanafunzi wake wakasikia.*
>
> *Wakafika Yerusalemu, naye akaingia ndani ya hekalu, akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza na kununua ndani ya hekalu, akazipindua meza za wabadili fedha, na viti vyao wauzao njiwa;*
>
> *Wala hakuacha mtu achukue chombo kati ya hekalu.*
>
> *Akafundisha akasema,* Ime. . . *haikuandikwa, nyumba ya* Baba Yangu *itaitwa* ile. . . *nyumba ya sala kwa mataifa yote? Bali nyinyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi.*
>
> *Wakuu wa makuhani na waandishi wakapata habari wakatafuta jinsi ya kumwangamiza; maana wali— maana walimwogopa, kwa sababu mkutano wote walishangaa kwa mafundisho yake.*
>
> Na kulipokuwa jioni *alitoka mjini.*
>
> *Na asubuhi,* (sasa hiyo ni siku nyingine), *walipokuwa wakipita waliuona ule mtini umenyauka toka shinani.*

Katika masaa ishirini na manne, muujiza ulikuwa umetendeka, baada ya Yeye kuuambia, "Mtu asile." Hakuna kitu, ilivyoonekana, kilitokea wakati huo; lakini, siku iliyofuata, ulikuwa umekauka.

> *Petro akakumbuka habari yake* akamwambia*, Rabi, tazama, mtini* ulioulaani *umenyauka.*
>
> . . . *Yesu* akamjibu, akawaambia, *Mwaminini Mungu.*
>
> *Amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni*

> *mwake, ila aamini kwamba hayo* asemayo *yametukia, yatakuwa yake.*
>
> *Kwa sababu hiyo nawambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu.*
>
> *Nanyi, kila msimamapo na kusali sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu.*
>
> *Lakini kama ninyi hamsamehi, wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu.* (Ina masharti).

52 Sasa ningetaka kusoma Yohana wa Kwanza 4:4.

> *Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na Mungu; nanyi mumewashinda, kwa sababu*. . .(sikizeni kwa makini). . .*yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia.*

53 Hebu nilisome tena sasa.

> *Ninyi, watoto wadogo, mwatokana na Mungu; nanyi mmewashinda,* (Yeye anazungumzia kuhusu mpinga Kristo) *kwa sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia.*

Vijina viwili, unaona, "yeye," kijina cha nafsi; "yeye" aliye katika dunia, na "Yeye" aliye ndani yenu. "Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia."

54 Sasa, na su—sura ya 28 ya Mathayo Mtakatifu, na aya ya 20.

> *Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi:*. . .*tazama, mimi nipo pamoja nanyi* siku zote, *hata ukamilifu wa dahari.*

55 Sasa kifungu kutoka katika hayo, usiku wa leo, ningependa kutumia hili kama fungu la maneno: *Yeye Aliye Ndani Yenu*. Na katika hili nataka kujenga imani, bila shaka, kwa ibada ya maombi. Na haraka tu. . .

56 Sasa, ni kama nilivyowaambia, nataka kuwasimulieni matukio yaliyotukia. Na kwa kawaida mimi hungoja mpaka nije ka—kanisani hapa, kusimulia matukio. Ndipo kama wengine wanataka kusikia, wanaweza kulisikia katika kanda. Lakini hungojea mpaka nifike humu.

Na kuna, haikosi, katika tukio hili ambalo nataka kuwasimulieni sasa hivi, kuna watu wengi hapa ambao ni shahidi wa haya, ndugu Wakristo. Mmoja ambaye alikuwepo, alikuwa Ndugu Banks Woods. Mwingine ambaye alikuwepo, alikuwa Ndugu David Woods. Mwingine, ambaye yuko hapa, alikuwa Ndugu Evans na mwanawe, Ronald. Mwingine aliyekuwepo, ni shemasi wetu mwaminifu, Ndugu Wheeler. Na mwingine, aliyekuwepo, alikuwa Ndugu Mann. Ndugu Mann

yupo, toka New Albany? Mhubiri wa Kimethodisti ambaye nilimbatiza katika Jina la Yesu Kristo, hivi majuzi, alikuwepo, pia, hili lilipotukia.

57 Imekuwa kwa muda fulani, kwa miaka michache, kwamba nilikuwa na mzigo mzito kifuani mwangu kwamba mimi... moyoni mwangu. Nilijisikia kana kwamba nimetenda kitu kibaya. Nami niliyachunguza maisha yangu, tena na tena na tena, kuona kulikuwa na kasoro gani. "Bwana, kama—kama nimetenda kosa lo lote, basi nifunulie tu, hilo kosa, nami nitakwenda na kulirekebisha." Lakini hakuna cho chote kingefunuliwa kwangu. Ningesema, "Je! nilimuudhi mtu fulani? Niliacha kitu fulani bila kukitekeleza? Nime...je! ninasoma vya kutosha? Ninaomba vya kutosha?" Nami ningesoma na kuomba. Na—na ninge—ningesema, "Nifunulie jambo hilo. Je! nilimdhuru mtu fulani, mahali fulani? Kama nimemdhuru, nitalirekebisha. Naomba tu unionyeshe; sitaki mzigo huu." Na kwa miaka mitano iliyopita, tangu niondoke uwanjani, kumekuwa na mzigo ulioning'inia moyoni mwangu.

58 Nimekwenda milimani. Nimekwenda ufukoni mwa bahari. Nimekwenda kila mahali, na kuomba na kuomba na kuomba, na haungeondoka. Nami nilifikiria kila kitu, kama nimetenda cho chote. Lakini huo, bado, haungeondoka; nilikuwa tu katika utumwa, namna hiyo.

Na ni ajabu sana kwamba huu uliondolewa wakati Ujumbe huu ulipokuja, unaona, asubuhi ya leo. Sasa, je! ilikuwa ni Mungu akiuzuilia kwa ajili ya huu? Sijui. Unaona, mimi... Mambo haya yote yalikuwa bongoni mwangu. Unaweza kuwazia kilicho ndani ya moyo wa mtu wakati unapovumiliana na hilo, unaona, kufikiria kuhusu yanayotukia; na, kujua, kuwaambia watu, ukijua kwamba baadhi yao wataelewa vibaya, na wengine watakwenda *hivi* na *vile*. Na unajua jinsi ilivyo. Na baadhi yao wataamini, na baadhi yao hawataamini. Na, huna budi kuvumilia hayo.

59 Unawezaje kulisema bila ya kuudhi? Unawezaje kulisema, hata lipate kutenda kazi? Unawezaje kulisema, kuwaonyesha watu kwamba wewe hu—huwaonei wao, kwamba unawapenda? Unawezaje kuwa mkali na thabiti, na bado mwenye upendo? Na, loo, utalileta je? Na halafu ole wangu kama sinileti! Unaona? Na ndivyo ilivyo. Unaona? Hilo, si ajabu, linakuweka katika wasiwasi na kuishiwa na nguvu.

60 Nilishuka kutoka—kutoka...nilipanda toka Arizona, kukutana na kundi la ndugu hapa, wanaokwenda kuwinda pamoja nami huko Colorado, kila mwaka.

Sasa, baadhi ya watu wameshangaa, "Kwa nini unakwenda mawindoni? Nini kinakufanya uende?"

Unaona, *hapa*, ninyi mnajaza, mimi ninamwaga; *huko*, ninajaza, kusudi nipate kumwaga. Unaona? Sasa, siendi kuwaua

tu wanyama. Mbona, enyi watu, mtu ye yote hapa anayekwenda pamoja nami, anajua kwamba ninapita mamia ya wanyama na hata kamwe siwagusi. Siwagusi.

61 Sasa, hapa si muda mrefu uliopita, nilianza kuwaua wanyama kwa ajili ya Wakristo wafanyi biashara, walipoinuka na kusema, "Billy, niulie fahali, niulie jike la mnyama, niulie kulungu, niulie *huyu*, au *yule, mwingine*." Ningetoka niende kuwaua wanyama, kulia na kushoto. Bwana alinisaidia ili niweze kuwaona na kuwapata wanyama, na shabaha nzuri sana, na kuwapiga risasi. Na—nao waliketi tu pamoja na kuzungumzia kuhusu biashara zao.

62 Ndipo Bwana akaniambia nisitende jambo hilo tena. Nami ni—nilijisikia vibaya kuhusu jambo hilo, kwa hiyo nilimwahidi Yeye singefanya hivyo tena. La. Nilisema, "Kama ni jambo la dharura na mtu fulani ana haja, nitafanya hivyo. Lakini kama hawahitaji, sitafanya hivyo." Kwanza hao watu, wana fedha za kutosha kununua nyama ya ng'ombe na kadhalika. Kwa hiyo kwa nini nifanye hivyo? Mwache mnyama aishi kama hutamtumia.

63 Kwa hiyo mimi huenda huko nipate kuwa peke yangu. Na mtu ye yote, anayepata kwenda nami kuwinda, anajua siwindi na mtu ye yote. Natoka kwenda peke yangu, kuwa peke yangu. Ningekwenda pamoja nao, tupate kuwa na ushirika usiku, tusimame mahali na kuomba, na kadhalika.

Lakini kulikuwepo na wahudumu wengine wengi kule. Kulikuweko, juu huko milimani mwaka huu, alikuweko Ndugu yetu Palmer. Naamini nimemwona mahali fulani hivi punde . . . Huyu hapa, ameketi hapa, Ndugu Palmer. Na Ndugu fulani jina lake Bob Lambert, alikuwepo hapa asubuhi hii, nilimsikia akipaza sauti mahali fulani. Nadhani bado yungali hapa. Na halafu alikuweko ndugu nanii . . . wana wawili wa Martin, nadhani wapo hapa. Wapo, wana wa Martin? Ndugu, Ndugu Martin. Ulinipigia simu juzijuzi, hilo lilikuwa zuri. Mvulana yule aliponywa, yule ndugu mhudumu.

64 Upo hapa, yule niliyemwombea, kwenye simu, juzijuzi? Ninasahau jina lake, toka chini huko Arkansas. Mkewe alinipigia simu; mtu yule alivimba ubavuni mwote, na homa kali, akifa. Mtu yule yule aliyeitwa, chini kwenye—Little Rock, au kwenye mkutano wa Hot Springs, akiketi mkutanoni.

Na ni jamaa mwenye sura nzuri. Kama yupo hapa, nadhani hatainuka sasa, hata kidogo. Lakini ninasahau jina lake. Siwezi kukumbuka jina lake. [Mtu fulani anasema, "Ndugu Blair."—Mh.] Blair. Ndugu Blair, Mtu fulani . . .

Vema, sasa, tukiketi katika mkutano huko Little Rock, wangapi walikuwepo, ninamaanisha, huko Hot Springs, wangapi walikuwemo mkutanoni? Na Roho Mtakatifu alimwita yule kijana akamwambia kwamba Ibilisi alikuwa akijaribu

kumfanya yeye kunikanusha mimi, kusema nilikuwa "nabii wa uongo." Na mtu yule alishuhudia kwamba ilikuwa ni kweli. Unaona ambalo Ibilisi anafanya? Mtu huyo haendi kwa madaktari. Haamini kwenda kwa madaktari. Lakini Shetani alijua ugonjwa huu utampata, naye angeweza kumuua papo hapo. Unaona? Kwa hiyo alikuwa akijaribu kumfanya anikanushe. Na Roho Mtakatifu, katika neema, alimwita na kumwambia asitende hivyo; mtu yule, akiwa mgeni, alimwambia asitende hivyo.

65 Na usiku wa juzijuzi, mkewe alinipigia simu akasema, "Ndugu Branham, ninaamini kwamba anakufa." Kasema, "Ame—amevimba kila mahali. Na, homa yake, nusura arukwe na akili." Kisha kasema, "Jambo la mwisho alilosema, 'Mwite Ndugu Branham."

Nikasema, "Una kitu cho chote, pochi yako ina leso?"

"La." Nilikuwa Tucson; yeye alikuwa Arkansas.

Ndipo nikasema, "Una yo yote?"

Akasema, naamini, "shali" yake.

Nikasema, "Sasa weka mkono wako juu ya shali hiyo, huku umeshikilia simu kwa mkono ule mwingine." Nami nikaomba na kumsihi Mungu amrehemu na kumkanusha adui yule.

66 Naye akaondoka akaenda akaiweka ile shali juu ya mtu huyo. Ndipo asubuhi iliyofuata, mtu huyo akanipigia simu.

67 Sasa, katika masaa yapatayo ishirini na manne, au chini ya hayo. Ndugu yetu wa thamani, bado sijamwona usiku wa leo, Ndugu Roy Roberson. Na wakati mmoja, mnajua, Ndugu Roy alikuwa kwa namna fulani mwanajeshi. Kama yuko hapa, na—natumaini ataelewa, kwa sababu mimi—mimi silaumu hilo. Lakini kila kitu ni kushurutisha utii, yeye alikuwa sajini Jeshini, mwajua, na inakubidi kwa namna fulani kuzoea kumshughulikia mtu kama wafanyavyo Jeshini. "Vema, mambo haya ya kiroho ni kwa ajili ya mtu mwingine," si yeye! Bali Bwana aliokoa maisha yake. Angekuwa maiti; walimweka huko wakidhani amekufa, kwa muda mrefu. Bwana alimponya; amemfuata tangu wakati huo. Bali mambo hayo yote ya kiroho, hakuyajua, na maono.

68 Na hapa si muda mrefu uliopita, wengi wanajua lile ono ambalo alipewa Ndugu Roy hata kabla ya mimi kwenda kule, kuhusu yeye akiniona mimi nikisimama juu ya mlima kule, katika Nuru ile, na Sauti ikitoka kwangu. Hilo liliondoa mashaka yote kwa Ndugu Roy.

69 Na usiku wa juzijuzi alishambuliwa vibaya sana mpaka akawa mgonjwa sana, na akapata homa kali sana, na kadhalika. Na daktari alikuwa amempa dawa, kila kitu, na basi haikumfaa kitu. Na hata alifikia mahali ambapo hata hangeweza kujisogeza

mwenyewe tena. Miguu yake na kadhalika ilikuwa, kama kwamba, imepooza.

70 Na maskini ndugu huyu ameumizwa vibaya sana kwa risasi, na vipande vya risasi kutoka kwenye bunduki ya themanini na nane, bunduki ya Kijerumani ya themanini na nane. Nayo—ilikuwa tu ile. . . Na nafikiri kikosi chote kilivawa, isipokuwa yeye, naye alikuwa pale amelipuliwa vibaya sana.

71 Na unajua nini kilitukia? Nilimwambia mke wake muungwana, Dada Roberson, ku. . . Akasema. . . nikasema, "Una cho chote hapo?"

72 Akasema, "Nina leso uliyoombea wakati mmoja."

73 "Nenda kailete." Nami nilikuwa Tucson, naye akaweka mkono wake juu yake, nikaomba na kukemea, na kusema, "Dada Roberson, itamwacha."

74 Kitu fulani kikaniambia pale, "Itamwacha. Sema hivyo!" Na mnamo nusu saa, homa ile ilimwacha; alikuwa jikoni, akitafuta chakula. Unaona? Unaona?

75 Ninachojaribu kusema, "Usife moyo." Usimruhusu Shetani akuambie ubaya kunihusu mimi; sababu ana mengi. Bali wewe shikilia matumaini hayo; sababu, usipoyashikilia, haitatendeka. Usiniangalie mimi, kama mwanadamu; mimi ni mwanadamu, nimejaa makosa. Bali tazama yale ambayo ninayosema kumhusu Yeye. Ni Yeye. Yeye Ndiye.

76 Tulipokuwa Colorado, unaona, tulipokuwa juu kule, tulirudi. Na kulikuwa kumekauka sana. Wanyama walikuwa haba. Ndugu Wheeler, Bwana alimbariki na kumpa—akampa mnyama mkubwa, nasi tulifurahia sana jambo hilo. Ilikuwa mara yake ya kwanza kuweko msituni akiwinda, na Bwana akambariki. Halafu nilikuwa nimempiga risasi mnyama mkubwa ambaye nimemtafuta kwa muda wa miaka ishirini, nimekuwa nikimtafuta. Mimi pamoja na Ndugu Banks tumemtafuta muda mrefu. Na nilipopiga. . . Nikilenga bunduki yangu huko kwenye nchi yenye joto, nikiileta kwenye nchi ya baridi, ilitanuka kwenye mpini, ingawa ilikazwa kwenye darubini. Na ililenga umbali wa inchi nyingi, na kumpiga yule mnyama, akisimama kati ya miti ambapo haikupaswa kumpiga; chini zaidi ya hapo, ambayo ingemuua mnyama yule pasipo maumivu katika sekunde moja. Bali ilimpiga juu sana, huyo, akaruka, ikatokea kwamba alianguka namna hiyo.

77 Na Billy alikuwa pamoja nami, naye akasema, "Hiyo imempata." Nami nilifikiria imempata, pia; bali nilipokwenda kule, haikuwa hivyo. Akasema, "Ulipiga mti." Niliangalia juu chini, hakukuwa na alama juu ya mti. Basi nikaendelea kumtafuta.

Kisha kukaja ishara ya ilani. Kulikuwa na watu wapatao mia moja, juu yetu kidogo. Na Ndugu Palmer na hao

wengineo ni shahidi wa jambo hilo. Na Ndugu Evans, hiyo ni kweli, alikuwepo; Ndugu Welch Evans na mwanawe, Ronnie. Ninaamini niliwapigia simu, muda mchache uliopita. Na wingi wa watu ulikuwa umepanda ukaenda juu yetu, wanayoita kambi ya ng'ombe juu kule, ambako macowboy hukaa na kupanda farasi, wanawabagua ng'ombe. Mimi mwenyewe nilikuwa nikikaa katika kambi ile na kuwachunga hao ng'ombe na kuwatenganisha.

78 Halafu basi, kwa hiyo, mle ndani, kulikuweko na yapata watu mia moja. Lakini mtu ye yote anajua, katika nchi ile, tufani ya thaluji inapotabiriwa, afadhali uondoke sasa hivi. Hiyo ndiyo sababu Ndugu Palmer na wengineo waliondoka mapema, kwa sababu walikuwa na motokaa isiyo na mbio sana, nao iliwabidi kuondoka hapo; sababu, hali ya hewa, uko pale, nawe unaweza ukakaa majuma kadha. Kwa hiyo walisema, "Tufani ya theluji inakuja," utabiri, magazeti, redio. Kundi baada ya kundi, karibu kila kitu kutoka kila mahali kule juu kiliondoka. Walikwisha ondoka, wakati huu, sababu walijua namna ya kutoka mle.

79 Lakini ndugu zangu walikuwa na leseni ya kulungu wawili, nao—nao hawakutaka kuondoka. Kwa hiyo ni—nikasema, "Vema, tutakaa." Lakini nilikuwa natazamia mkutano, mnamo muda wa kama siku sita, na ilinibidi kurudi Tucson.

80 Kwa hiyo maskini mke wangu, mimi—tangu tuoane ni miaka ishirini na miwili. Na miaka ishirini na miwili, kwenye sikukuu ya ukumbusho wetu, nimekuweko kule juu kila wakati; inatokea tu kwamba wakati huo hufika nikiwa kule. Kwa hiyo ni—nina mahali padogo ninapoenda kuombea, na ilionekana kama mahali nilipokuwa nimempeleka.

81 Mwajua, nilitengeneza namna ya kitu kidogo, unajua. Sikuwa na hela za kutosha kwenda mawindoni na fungate yangu, kwa hiyo mimi—mimi—mimi kwa namna fulani nilimchukua mke wangu kwenye ziara ya kuwinda kwa ajili ya fungate. Kwa hiyo tulikuwa huko New York, nami ninakumbuka nikimsaidia yeye kuruka magogo na kadhalika, kufikia mahali. Na nilipata mahali padogo nje kule, sikuzote humfikiria yeye niendapo pale katika sikukuu ya ukumbusho wetu. Oktoba ishirini na tatu ndipo msimu huo unapoanza kule. Na, miaka ishirini, sijawa nyumbani, sikuzote juu kule.

82 Kwa hiyo siku hiyo ilikuwa sikukuu ya ukumbusho wetu. Na Ndugu Mann. . . Nikasema, "Sasa kama ninyi ndugu. . ." Nikasema, penye moto, asubuhi ile, "Sasa kama. . ." Usiku ule, hasa. "Kama ninyi nyote mnataka kukaa sasa, kumbukeni, tungeweza kuwemo humu mwezi mzima." Sababu nimeona futi ishirini na mbili za theluji zikianguka katika muda mdogo, usiku mmoja. Ni kwamba tu, ungetoka uende kule, u mkavu tu na unapendeza; na asubuhi inayofuatia, theluji ilipata kina *hiki*, juu, pengine juu ya hema lako. Kwa hiyo basi nikasema. . . Na

basi unakaa hapo mpaka hiyo iyeyuke. Kwa hiyo uko kama maili kumi na tano hadi ishirini kule nyuma nyikani. Na kwa hiyo basi nikasema . . . Na kama inakuwa dharura, bila shaka, wanatuma helikopta wanakutoa huko. Lakini, kwa kawaida, wao tu . . . na hakuna mtu anayeangamia, itawabidi tu kungojea mle.

83 Kwa hiyo kila mtu hutawanyika mara tu wanaposikia tangazo hilo la redio, utabiri, hasa. Kwa hiyo tulikuwepo nyuma kule, nami nikasema, "Sasa amueni. Kama mnataka kukaa, nipo hapa kuwinda pamoja nanyi, nami nitampigia simu mke wangu nimwambie, 'Nakutakia Sikukuu Njema!" Lakini nikasema, "Basi, kwa hiyo, pia mimi nita . . . nita . . . tuta—tutanunua vyakula, sababu pengine itatubidi kukaa humu." Tulikuwa tumemaliza mkate wakati huo. Nami sitaki kuona vitumbua tena kwa muda mrefu, hayo maandazi! Kwa hiyo, basi, nilikuwa nikiyala huko Canada, kwa yapata siku ishirini na moja, na hakika yalinichukiza. Na kwa hiyo basi nilitaka kununua mkate.

84 Kwa hiyo walisema tu wanataka kukaa. Kwa hiyo hapakuwa na la kufanya . . . kukaa. Lakini mimi na Ndugu Mann tukatoka, basi tukashuka tukaenda kule nami nikanunua vyakula. Nami nikampigia simu mke wangu, na simu haingejibu. Hakuna mtu aliyejibu; kwa hiyo nikangojea kama saa moja mpaka tukanunua vyakula, tukarudi, nikapiga simu, hakujibu. Basi ikanibidi kumpigia Dada Evans.

Naamini Dada Evans yuko hapa. Basi nikamwambia . . . Ndiyo, Ndugu Evans na Dada Evans wako hapa.

85 Kwa hiyo nilimwita Dada Evans, kwa ajili ya Ndugu Evans, na nikamwambia. Akasema, "Nitampigia Dada Branham nimwambie." "Nakutakia Sikukuu Njema," bila shaka, unajua. Kwa hiyo, lakini alikuwa amekwenda madukani, kuwanunulia watoto vyakula.

Halafu tukarudi. Na asubuhi iliyofuatia, nini kilikuweko angani ila mawingu. Haikuwa imenyesha juu kule msimu wote wa kupukutika majani, na kulikuwa kukavu sana. Nao walikuwa wamezidisha msimu wa kuwinda, siku chache za ziada, kwa ajili ya ukame.

86 Naam, nikawaambia hao ndugu asubuhi ile, "Sasa, tone la kwanza la mvua likianza kuanguka, theluji ya kwanza, manyunyu ya kwanza ya theluji, cho chote kile, kimbieni kambini haraka mwezavyo, kwa sababu mnamo dakika kumi na tano huwezi kuona mkono wako mbele yako. Unaona? Na itavurumisha na kuvuruma, nami sijali jinsi gani unaifahamu vizuri nchi, uta—utakaa papo hapo, nawe utaangamia. Kwa sababu wakati mwingine hata huwezi kuvuta pumzi, mvua ya theluji ikivuma kasi sana, na, utakufa papo hapo." Nami nikasema, "Mara tu mvua ya theluji ianzapo, kimbieni kambini haraka mwezavyo, sijali mlipo."

87 Vema, nikasema, "Pandeni mwende huku na mkae katika mabonde haya yaliyo na kina kirefu, nami nitapanda juu kule na kuviringisha mawe kilimani, na kadhalika, kuwatisha kulungu watoke kule juu, niwafukuze watelemke, mkachague muwatakao."

88 Kwa hiyo nikaanza kupanda juu, na karibu wakati nilipofikia mahali tunapoita "tandiko," mahali padogo pale ambapo mimi sikuzote huvuka kwenda mahali paitwapo "Quaker Knob," katikati ya Continental Divide kule, juu sana. Nami nilipofika karibu na tandiko hili dogo, hili . . . mawingu yakizidi kuwa meusi. Hapakuwepo na gari lililobakia, ni sisi tu kule juu, kadiri . . . na cowboy aliyeko kambini. Kwa hiyo ha—hali ikazidi kuwa mbaya. Kwa hiyo, mnamo dakika chache, ilianza kunyesha. Naam, nikachukua bunduki yangu na kuiweka chini ya koti langu, darubini isije ikapata ukungu na—na mpini ukalowa maji; huenda nikakumbana na dubu au kitu fulani, nikirejea, kwa hiyo mimi—mimi nikashikilia darubini ya bunduki yangu jinsi *hiyo* na kuketi chini ya mti, kidogo. Nami nikaketi pale, na nikaomba. Nikasema, "Bwana Mungu, Wewe u Yehova aliye Mkuu, nami nakupenda Wewe."

89 Matukio mangapi nimeyapata! Nikawaonyesha hao ndugu, Ndugu Palmer na wengineo, sehemu zile. Ambako, yule tai, mnajua, nilimwona akiinuka juu siku hiyo, unajua, na jinsi . . . Sehemu zile ambako yote yalitukia mle ndani. Ni jambo la kusisimua kwangu, kule. Nimekuwa na matukio mengi makubwa na Bwana wangu, juu kwenye hiyo milima. Kwa hiyo huwezi kamwe kwenda kule bila ya kumwona Yeye; Yeye yuko tu kila mahali.

90 Kwa hiyo basi nilipo—nikaketi pale, ndipo mvua ya theluji ikaanza, na upepo ukivurumisha, namna hiyo. Nami nikasema, "Vema, najua njia ya kushukia, lakini afadhali niondoke hapa sasa hivi." Kwa hiyo nikasema . . .

91 Basi niliangalia kule chini, na sikuweza hata kuona sehemu za chini tena; hayo mawingu yakizungukazunguka na kuvurumisha, na mvua ya theluji ikivuma. Na hiyo hapo, tufani! Ilitabiriwa kwa siku nyingi, "Tufani kubwa inakuja!"

92 Ndugu Tom yupo hapa. Ndugu Tom Simpson, akija kutoka Canada, aliusikia huo utabiri, naye alishauriwa asipitie sehemu hiyo ya nchi, sababu utabiri huu ulisema, "Itakuwa tufani." Uko wapi, Ndugu Tom? Nafikiria hivyo, naam, papa hapa. Naye . . . Tufani ilikuwa inakuja! Kila mtu alikuwa amejiandaa kwa ajili yake.

93 Naam, nikairudisha bunduki yangu chini ya shati langu, hivi, shati langu jekundu, nikaanza kushuka mlimani. Nami nilipoanza, nilifikia kama nusu maili kutoka kwenye lile tandiko; na, loo, jamani, na matone makubwa ya theluji, *hivyo*, na upepo ukivurumisha, mlimani, na kuvuma. Sikuweza tena

kuona sehemu za chini. Niliweza kuona kama futi ishirini mbele yangu, au thelathini. Nami nilikuwa ninashuka kwenda moja kwa moja chini ya hiki kidogo, tulichokiita "kijigongo cha nguruwe," kigongo kidogo, kisha nikafika kwenye kijito, ndipo nilijua yanipasa kufuata hicho kijito, na mahali pa kwenda, kama hali ingaliharibika mno.

94 Na kwa hiyo basi nikaanza kushuka, na nikafika yapata nusu yake, na Kitu Fulani kikaniambia, wazi kabisa kama mnavyonisikia mimi, "Simama, na urudi nyuma!"

95 Vema, nikawaza, "Nilikuwa ninawazia jambo gani? Pengine ni akili zangu tu." Nami singeweza kupiga hatua nyingine kwenda mbele.

96 David alikuwa amenitengenezea sambusa asubuhi ile, nami nafikiri alijaribu kulipiza kisasi kwa kuwa nilimtengenezea baba yake moja, wakati mmoja, ya kitunguu na asali, hivyo tu ndivyo tulivyokuwa navyo. Kwa hiyo alinitengenezea sambusa yenye pilipili na, loo, sijui yote ilikuwa nini, kilichofungiwa mle ndani! Na nilikuwa nacho katika shati langu, na kililowa maji kwenye shati langu. Nikawaza, "Nitasimama tu nile hii, na pengine nita . . . Nitapata nafuu basi." Kwa hiyo nikaitoa ile sambusa, mnamo saa nne, nami nikaanza kuila ile sambusa. Na nilipokuwa nikiila ile sambusa, niliwaza, "Sasa nitapata nafuu."

Ndipo nikaanza kwenda mbele, lakini Kitu Fulani kikasema, "Rudi ulikotoka!"

97 "Nirudi nipitie katika tufani ile, nusu maili au zaidi kule nyuma mlimani, kwenye msitu ule wenye giza?" Ambako, ni vigumu kwako kuona umbali wa kinanda kile! Lakini ninazeeka, nami nimekuwa Mkristo sasa kwa miaka thelathini na mitatu; nami najua, haidhuru nini, hata lionekane la kipuuzi jinsi gani, mjali Bwana, tenda asemalo Bwana.

98 Nami nikageuka nikarudi kwenye lile tandiko, nikirudi kwa kupapasapapapasa. Lo, mvua ya theluji ilikuwa inazidi kunyesha; giza lilikuwa linazidi kuingia. Nami nikaketi chini kule, na nikaweka koti langu hivi, au nikafunika darubini kwa shati langu tena; nikaketi chini. Nikawazia, "Ninafanya nini hapa? Hivi kwa nini nimerudi hapa tena?"

99 Nami nikangoja dakika chache. Ndipo nikaanza kusimama tena, na waziwazi tu jinsi ningelitaka kusikia, Sauti ikasema, "Mimi ni Muumba wa Mbingu na nchi! Nazifanya pepo na mvua." Nikatoa kofia yangu.

100 Nikasema, "Ewe Yohava Uliye Mkuu, je! huyo ni Wewe?"

101 Yeye akasema, "Mimi Ndimi niliyezifanya pepo kutulia juu ya bahari. Mimi Ndimi niliyeyatuliza yale mawimbi, niliziumba mbingu na nchi. Si mimi Ndiye niliyekwambia useme na wale, kwa ajili ya kindi, na wakawepo? Mimi ni Mungu."

102 Sasa, sauti inapozungumza nawe, chunguza Maandiko. Kama si ya Kimaandiko, iache; sijali ni wazi jinsi gani, achana nayo.

103 Nikasema, "Ndiyo, Bwana."

104 Yeye akasema, "Nena na pepo hizo na tufani ile, nayo itaondoka." Sasa, Biblia hii ipo mbele yangu, ambapo uhai wangu umo katika Hiyo.

105 Nikainuka, nikasema, "Siishuku Sauti Yako, Bwana." Nikasema, "Mawingu, theluji, mvua, mvua ya theluji, ninachukizwa na kuja kwenu. Katika Jina la Yesu Kristo, rudini makwenu! Nasema kwamba jua lazima lichomoze mara moja na liangaze siku nne, mpaka safari yetu ya kuwinda imekwisha nami nimeondoka pamoja na ndugu zangu."

106 Ilikuwa tu inafoka kwa nguvu, ikaondoka, "Whoooossssh," namna hiyo. Na ikaanza kwenda, kwenda "Whoosh," halafu ikaenda, "whi, whi, whi, *whi*." Ikanyamaza!

107 Nikasimama kimya kabisa. Ndugu zangu kule juu, na wakishangaa nini kilikuwa kinatukia. Na ile mvua ya theluji na mvua vikakoma. Kukaja uvumi wa upepo ukishuka milimani, ukayainua yale mawingu, na moja likaenda *hivi*; mashariki, kaskazini, magharibi, na kusini. Na, mnamo dakika chache, jua lenye joto lilikuwa linawaka vizuri. Hiyo ni kweli! Mungu anajua hiyo ni kweli!

108 Nilisimama tu pale, nikiangalia kila upande; huku nimevua kofia yangu, nikitazama. Ni...Hebu wazia...Nikafa ganzi, mwili mzima.

109 Nikawaza, "Mungu yule yule wa Maumbile, yote yako mikononi Mwake. Yeye ananiambia nini?"

110 Nami nikaokota bunduki yangu, nikapangusa darubini, nikaanza kurudi, kushuka kilimani. Na Kitu Fulani kikaniambia, "Kwa nini usipunge hewa Nami katika nyika hii, utembee Nami?"

111 Nikasema, "Ndiyo, Bwana, kwa moyo wangu wote; ni moja ya mambo makuu kupita yote ningeweza kutenda, ni kutembea na Wewe." Kwa hiyo nikaweka bunduki yangu kwenye bega langu, nami nikaanza kutembea huko; kamwe shoka halijaugusa, mwitu pasipokanyaga mtu, nikitembea mle.

112 Na nilipofanya hivyo, kutembea, kule katika miburuzo hii ya wanyama, nikajisikia kama, "Naamini nitakwenda mahali ambapo...jana ilikuwa ni sikukuu ya ukumbusho wa ndoa yetu, nami nitasimama pale dakika chache; kama salamu ndogo kwa Meda, ambako kuna vifutu wengi watetemekao, juu kwenye kiduta kidogo." Nami nikasema, "Naamini nitatembea juu kule, kwa kuheshimu sikukuu ya ukumbusho wetu kidogo. Halafu nitashuka nirudi upande huu mwingine, katika msitu huu wenye giza, na kutembeatembea, na nizunguke hapa karibu, kuelekea

Corral Peaks, ndipo nishuke nirudi upande ule." Nikitembea tu na kufurahi.

113 Nilikuwa nikisema, "Baba, ninajua Wewe unatembea pamoja nami. Na ni heshima jinsi gani; hakuna mtu aliye mkuu zaidi ningeweza kutembea pamoja naye; Mungu yeye yule hasa!" Na joto lile la jua!

114 Hata wakati nilipotoka milimani. Nilisimama kwenye vituo vya mafuta, nami nikasema, "Ni siku ya kupendeza!" Siku tatu baadaye. Haikunyesha kamwe katika sehemu ile ya nchi mpaka siku zile nne zilipokwisha. Jua liliwaka kila siku. Hiyo ni kweli, ndugu zangu? [Ndugu wanasema, "Amina."—Mh.] Unaona? Hata hamna wingu angani.

115 Basi nikafika kwenye kituo cha mafuta, nikasema, "Hakika ni siku ya kupendeza."

"Ndiyo, ni ya kupendeza!"

Nikasema, "Ukame umezidi sana."

116 Kasema, "Ni jambo la ajabu!" Huyu mtumishi akasema, akasema, "Unajua, walituambia tutapata tufani kuu, lakini kwa ghafla ilikoma!"

117 Nikashuka, kwenye mpaka wa New Mexico. Mimi na Billy, mwanangu, tulienda mahali padogo pale kununua. . .asubuhi tuliyoondoka, nami nikasema, "Hakika ni siku ya kupendeza."

"Ndiyo, inapendeza!"

Nikasema, "Inaonekana ukame umeshika sana."

"Ndivyo imekuwa!"

Nikasema, "Wewe ni mwenyeji?"

118 Kasema, "La, ninatoka Wisconsin," au mahali fulani. Kasema, "Nimekuwa hapa yapata miaka ishirini, kwa hiyo nadhani ungeweza kupaita nyumbani."

119 Nikasema, "Basi wewe u mwenyeji, nadhani." Kwa hiyo nikasema, "Ndiyo, bwana," nikasema, "yaonekana kumekuwa na vumbi sana."

120 Akasema "Wajua, jambo la kushangaza sana lilitukia!" Kasema, Ilitabiriwa kwamba tungepata tufani, theluji nyingi; na kwa kweli ikaanza, kisha ikaondoka!"

121 Nikasema, "Usiseme," kwa utulivu sana.

122 Ndipo nikaja nyumbani. Naye Ndugu Tom akasema alikuwa ameambiwa asiende huko, tufani yaja. Naye akaja moja kwa moja kupita nchini, bila hata tone la mvua au cho chote kile! Yeye yuangali Mungu, unaona, kama vile tu Yeye alivyowahi kuwa. Unaona?

123 Nikiwa ninatembea juu kule, nilikuwa ninatembea. . .Sasa, sehemu hii, natumaini mke wangu hatapata kanda hii. Unaona? Lakini nitawaambia jambo fulani. Na, sasa, si—siwaambii. . .

Nitawaambia tu Kweli, unaona, na hiyo ndiyo njia pekee ya kulitenda. Mara nyingi nimeshangaa kwa nini hakulalamika kuhusu mimi kwenda kwenye safari hizi wakati wa sikukuu ya ukumbusho wetu. Unajua nilichoamua akilini mwangu? Nilisema, "Kuna watu wengi sana nyumbani. Na pia mimi sikuzote, unajua, nina wasiwasi. Na kila kitu ninachozungumza, ninachotaka kukizungumzia, ni Mungu, Biblia, au kitu fulani. Pengine yeye hufikiria tu ni mapumziko madogo kwake. Huniacha niondoke kwa siku chache, kwenda kuwinda." Mimi, nikitembea mle, huku kwa sehemu nikifikiria kuhusu hilo.

124 Kwamba, mimi ni . . . mimi, nitamwomba msamaha, na nina—nimemsihi Mungu kunisamehe kwa mawazo kama hayo. Sababu, nilikuwa ninatembea mle, nikawaza, "Vema, anafikiri . . . Vema, jamani! Yeye, yeye ni mfanya kazi, unajua, na—na saa zote wakati anapokuwa jikoni au mahali fulani huko kwenye . . . "

125 Na kila mmoja wenu anamjua yeye, huo mtambo wa kufulia nguo unatenda kazi saa zote. Na kwa hiyo ningetoka, ningemvuta; nikasema, "Usiwe unafua namna hiyo. Zungumza nami. Unaona, ninakupenda. Nataka uniambie jambo fulani; niambie na wewe unanipenda, pia."

126 Akasema, "Naam, unajua nakupenda," mara anaendelea kufua kwa bidii kama alivyowahi kufanya.

127 "Sitaki wewe ufanye hivyo. Nataka uje hapa uketi karibu nami."

128 "Jamani, Bill, nina kazi nyingi sana za kufanya!"

129 Nami nikawaza, "Vema, unaona, nikipanda kuja huku, anapata muda wa kufanya kazi yake." Nikiwa ninatembea kule, nikiliwazia hilo.

Sasa, kumbuka, nimeweka Biblia hii hapa ili muone kwamba niko mbele ya Neno.

Nilipokuwa ninatembea, kitu fulani kilinipata. Kama ningeanza . . .

130 Kwanza, nilikuwa ninafikiria kuhusu wakati nilipomchukua kule juu kwa fungate. Alikuwa maskini, msichana mrembo, mwenye nywele nyeusi, na macho ya kahawia, nami nilikuwa nikimpandisha juu ya magogo haya, unajua, na kila kitu, na kujaribu kumpeleka juu kule mahali ambapo niliva dubu. Nami nilitaka kumwonyesha mmoja, na kwa hiyo . . . mahali nilipompata dubu huyu. Naye alivaa viatu vyangu vya cowboy. Na hiyo ni kama miaka ishirini na miwili, au miaka ishirini na mmoja kabla ya hapo; miaka ishirini na miwili, naamini ilikuwa hivyo, iliyopita. Tulifunga ndoa mwaka wa 1941. Nami nilikuwa ninambeba, unajua, juu ya magogo haya.

131 Basi nikawaza, "Sasa, maskini mtoto wa watu, kwa kunivumilia, amepata mvi." Naam, nikawaza, "Vema," na

nikafanya . . . [Ndugu Branham anakohoa ili azungumze vizuri—Mh.] Nami sikuwa nimenyoa ndevu kwa siku chache, nami nikaona nilikuwa na mvi, pia! Na niliona ndevu zangu zikitokeza nje hapa, zina mvi, basi nikawaza, "Mzee, uko karibu kwisha sasa. Unaona, wewe, iwapo utafanya jambo lo lote, afadhali uharakishe. Unazeeka, pia." Unaona?

132 Na kwa hiyo nilipokuwa nikiendelea namna hiyo, kitu fulani kilitukia. Mara, katika kila hatua, tabia, nilikuwa mvulana, niliwaza kama mvulana. Nami nilikuwa nimekiinamisha kichwa changu chini, kisha nikainua macho yangu. Na waziwazi kabisa kama nilivyowahi kumwona, huyo hapo amesimama mbele yangu huku ameinyosha mikono yake. Nami nikatulia; nikapangusa uso wangu. Nikatazama. Nikasema, "Meda, ni wewe, Mpenzi?"

133 Nikatazama hapa, nikawaza, "Sasa kumetukia nini?" Nami nikawaza, "Ndiyo, ninatembea pamoja Naye." Na hapo ikabadilika, nikarudi kwenye uzee tena, na lile ono lika—likaniacha.

134 Nami nikasimama; nikatoa kofia yangu tena, nikaiweka kwenye moyo wangu. Nikasema, "Yesu, moyo wangu umelemewa sana, kwa miaka kadha. Hainilazimu kukuambia Wewe kwamba nimelemewa. Nimetubu, nimetubu, nimetenda kila nijuacho. Basi kwa nini mzigo huu hauniachi?"

135 Nami nikaanza tu kutembea. Basi nilipokuwa ninakwea kilima hiki kidogo, yapata tu yadi thelathini, arobaini mbele yangu; nilianza kukwea kilima hiki kidogo, nikaanza kujisikia mnyonge sana. Na palikuwa na kifutu mdogo, mwenye urefu upatao inchi kumi, akaja na kufanya kama L, halafu akapanda juu tena. Na nilipofika pale tu, nilijisikia mnyonge sana nilikuwa ninapepesuka. Kwa hiyo mimi . . . nilikuwa nimeivaa kofia yangu tena. Nami nililaza tu kichwa changu juu ya hii; ilinichukua vizuri sana, kulaza kichwa changu papa hapa juu ya huyu kifutu mdogo atetemekaye, hivi. Hasa ni mtakawa. Ni kama, unaonekana kama mchokochole, unaona. Na ni . . . nilijiegemeza tu pale. Nami nilikuwa tu nimesimama pale nimeinamisha kichwa changu, jua lile lenye joto likinipiga mgongoni. Ndipo nafikiri, "Mungu yeye yule hasa, ambaye aliondosha mvua ile na upepo ule!"

136 Nami nikasikia kitu fulani kikifanya, "pat, pat, spat."

137 Nikawaza, "Ni nini hicho?" Maji yote yemepeperushwa. Jua limechomoza. Hiyo sauti ya spat ni nini? Nikaangalia chini; ilikuwa ni maji yakitoka machoni mwangu, yakichuruzika kwenye ndevu zenye mvi na kuangukia kwenye majani makavu ambayo Mungu amekausha, yakiwa yako mbele yangu. Nami nilisimama tu pale *hivi*, nimeegemea kwenye mti. Mkono wangu, mkono *huu* chini, na kichwa changu kimeegemea kwenye mti,

mkono kwenye kamba ya bunduki *hivi*, nimesimama pale, nikilia.

138 Nikasema, "Mungu, sistahili kuwa mtumishi Wako." Kisha nikasema, "Na, ninasikitika, ni—nilifanya ko...nimefanya makosa mengi. Sikukusudia kufanya makosa, Bwana. Umekuwa mwema sana kwangu."

139 Macho yangu yakafumbwa; nami nikasikia kitu kikifanya, "kishindo, kishindo, kishindo, kishindo."

140 Nikainua macho yangu, ndipo wakaja kulungu watatu wakasimama papo hapo mbele zangu. Basi nikawaza, "Huyo hapo wa Ndugu Evans, wa Ndugu Woods. Na hao hapo wale kulungu watatu, unaona, wale tu ambao nawatafuta." Nikainuka mara moja; nikachukua bunduki yangu. Nikasema, "Siwezi kufanya hivyo. Nilimwahidi Mungu kwamba singefanya jambo hilo." Unaona? "Nilimwahidi Yeye singefanya jambo hilo."

141 Ndipo kitu fulani kikaniambia, "Lakini huyo hapo!"

142 Nami nikawaza, "Ndiyo, Sa-...Hilo ndilo m—mtu fulani alilomwambia Daudi, wakati mmoja, 'Mungu amemweka, nikasema, mikononi mwako!" Unajua, Mfalme Sauli.

143 Kisha Yoabu akamwambia, akasema, "Muue! Huyo hapo amelala!"

144 Naye akasema, "Mungu apishe mbali nimguse masihi Wake."

145 Na wale kulungu walisimama pale wakiniangalia. Kisha nikawaza, "Hawawezi kutoroka. Hawana njia ya kutoroka. Hawako yadi thelathini toka nilipo mimi. Nami nina bunduki hii, nimesimama hapa, na hao hapo kulungu watatu. Hasha, siwezi kufanya hivyo. Si—siwezi kamwe." Alikuwa kulungu jike na watoto wawili wakubwa. Kwa hiyo si—si—singeweza kuchukua bunduki ile. Nikasema, "Siwezi." Si—sikusogea kamwe. Nilikaa tu pale. Nikasema, "Siwezi kufanya hivyo, sababu nilimwahidi Mungu singelitenda. Ingawa, hao ndugu, wao ha—hawawahitaji hao kulungu. Unaona? Si—siwezi kutenda jambo hili. Siwezi kulitenda kamwe."

146 Na jike lile likaja, likanisogelea. Sasa sikilizeni, kulikuwa na watu mia moja wakiwafyatulia risasi juu kule, kwa siku nne au tano. Wanashtuka? Ishara ya kwanza nyekundu...Nami nilivaa shati jekundu, kofia nyekundu. Ishara ya kwanza, huwa wamekwisha kwenda; bali walikuwa wamesimama pale, wote watatu, wakiniangalia moja kwa moja.

147 Nikasema, "Mama, chukua watoto wako mwende mwituni. Mko mikononi mwangu. Mimi...Uhai wenu uko mikononi mwangu, lakini sitawadhuru. Nilimwahidi Mungu kwamba nisingewadhuru." Unaona? Naye akasogea karibu. [Ndugu Branham anagonga mara mbili kwenye mimbara—Mh.]

Angeniangalia. Wote wakasongea karibu, mpaka wakaja karibu sana hata wangeweza kula, kama ya mkini, toka kwenye mikono yangu. Wao, na upepo ukipuliza moja kwa moja juu yao. Kwa hiyo akageuka, akarudi nyuma hatua chache, hao wote watatu.

148 Na huyu hapa anarudi tena, akasogea karibu sana nami. Sikusogea kamwe; nilisimama tu pale. Nikasema, "Enendeni zenu mwituni; naupenda, pia. Ishini! Mnaona, uhai wenu uko mikononi mwangu, bali sitawadhuru. Msingeweza kukwepa. Mnajua msingeweza." Naweza kuwauwa hao wote watatu katika sekunde moja hivi, sekunde tatu, kwa vyo vyote, haraka tu niwezavyo kulenga risasi; nao wasingeweza kukwepa, wakisimama karibu sana nami. Unaona? Nami nikasema, "Sitawaua. Nendeni zenu, mkaishi." Nami nikasimama pale. Wakaanza kuondoka, wakaenda mwituni.

149 Nikapangusa uso wangu namna *hiyo*, mara kitu fulani kikatukia. Sauti ikanena, waziwazi tu, kutoka kwenye hizo mbingu za samawati, hakuna hata wingu. Yote yametukia yapata tu…muda mfupi tu. Na Sauti ikanena, ikasema, "Umekumbuka ahadi yako, siyo?"

150 Nikasema, "Ndiyo, Bwana."

151 Yeye akasema, "Nitakumbuka Yangu, pia. 'Sitakuacha kamwe wala sitakupungukia.'" Ule mzigo ukaondoka moyoni mwangu. Haujakuwepo mle tangu wakati huo; naomba usiwepo tena.

152 Halafu nikaja Tucson. Ajabu ni kwamba, sijawahi kamwe kuwa na matukio mengi jinsi hiyo, tangu niliposhuka nikaja huku. Na—naamini ilikuwa ni Mungu akishikilia kwa ajili ya saa hiyo. Naamini wakati umekaribia sasa, kwa jambo fulani kutendeka.

153 Laiti tungelipokea Kweli hii! Sasa hebu kidogo. Laiti tungelitambua Andiko hili linamaanisha nini!

> …*yeye aliye ndani yenu* ni mkuu *kuliko yeye* aliye *katika dunia.*

Hatuwezi kulielewa Hilo, hata hivyo tunasema tunaliamini Hilo. Nasi twajua Hiyo ni Kweli, lakini kwa kweli hatulifahamu.

> …*yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye* aliye *katika dunia.*

Ni kitu gani kilicho ndani yako, ambacho ni kikuu? Ni Kristo, mtiwa mafuta! Mungu, ambaye alikuwa ndani ya Kristo, yuko ndani yako. "Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia."

154 Basi kama Yeye yuko ndani yako, si wewe tena unayeishi, ni Yeye anayeishi ndani yako. Unaona? Si kuwaza kwako, kile ungewaza kuhusu Hili; ni kile Yeye alichosema kuhusu Hili. Unaona? Basi, kama Yeye yuko ndani yako, Yeye kweli asingekana alilosema Mwenyewe. Asingeweza kufanya hivyo.

Bali Yeye atatimiza alilosema Mwenyewe, Naye anajaribu kumpata mtu yule ambaye Yeye anaweza kujidhihirisha Mwenyewe kupitia kwake.

155 Sasa, hilo halimaanishi Yeye yambidi alitende hilo kwa kila mtu. Katika wakati ule Musa alipowaongoza wana wa Israeli, alikuwepo mmoja, huyo alikuwa Musa. Wengine wao walifuata tu Ujumbe. Unaona? Baadhi yao walijaribu kuinuka wapate kuigiza, ndipo Mungu akasema, "Jitengeni," ndipo akawameza wao. Unaona? Unaona?

156 Sasa, lakini, "Yeye aliye ndani yako ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Mungu ndani yako, kama Yeye alivyokuwa katika Yesu Kristo. Kwa sababu, yote aliyokuwa Mungu, Yeye aliyamimina katika Kristo; na yote aliyokuwa Kristo, Yeye akayamimina katika Kanisa. Unaona, huyo ni Mungu ndani yako, "Yeye aliye ndani yako."

157 Si ajabu pepo na mawimbi vilimtii Yeye, vilitii Maneno Yake; vilitii Maneno Yake, kwa sababu Hilo lilikuwa Neno la Mungu kupitia Kwake. Yeye alikuwa mtu; lakini Yeye alikuwa Neno, lililofanyika mwili. Unaona? Na Yeye aliponena, ilikuwa ni Mungu akinena kupitia midomo ya binadamu. Unaona? Si ajabu pepo na mawimbi . . . Yule Muumba hasa, aliyeumba pepo na mawimbi, alikuwa ndani Yake. Sasa, wazia jambo hilo! Fikiria kwa makini sasa, kabla sijafikia wakati huu wa kufunga. Si ajabu pepo walikomeshwa kwa Neno Lake! Ilikuwa ni Mungu ndani Yake. Ilikuwa ni Mungu katika Kristo. Pepo walikomeshwa. Si ajabu wafu, ambao walikuwa wanayarudia mavumbi, wasingeweza kukaa mle, kwa Neno Lake! Kwani, Yeye alikuwa Neno.

Yeye alimwambia Lazaro, baada ya kufa na kunuka, siku nne; uso wake, pua, vimebonyea, katika muda wote huo. "Lazaro, njoo huku!" Na mtu, aliyekufa, akasimama kwa miguu yake. Kwa nini? Ilikuwa Mungu. Yeye aliyekuwa ndani ya Kristo alikuwa Mungu. Wafu hawakuweza kusimama katika Uwepo Wake. Ilikuwa Mungu katika Kristo.

158 Pepo, sasa, kumbuka, Mungu aliumba pepo; ni hewa. Mungu aliumba mawimbi; ni maji. Lakini Ibilisi alipoingia ndani yake, aliyavuruga, kuleta uharibifu. Mungu aliwaumba watu, kuwa wana wa Mungu, lakini wakati Ibilisi anapowaingia, unaona, ni masumbufu. Sasa, huyo alikuwa Ibilisi aliyeingia katika pepo ambazo zilisababisha tufani ile. Je! Muumba, aliyeumba upepo, asingeweza kusema, "Rudi nilikokuumbia."

Je! huyo si Muumba yeye yule aliyekuwa amesimama kwenye kilima cha Colorado juzijuzi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Unaona?

Je! huyo si yeye yule Ambaye aliweza kuchukua kipande cha samaki na kukivunja, na kipande kingine kikakua juu yake? Yeye kwa kweli haikumlazimu awe nacho. Yeye angeweza kukinena.

Je! huyo siye Muumba yeye yule aliyeumba wale kindi? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi, Yeye aliyekuwa katika Kristo yumo ndani yetu, unaona, kwani Huyo anatenda kazi zile zile Yeye alizotenda, jambo lile lile.

Wafu hawakuweza kusimama katika Uwepo Wake, kwa Neno Lake.

159 Angalia, tunazo taarifa tano zilizothibitishwa rasmi, za watu "waliokufa," na Bwana akitoa ono, na kuwaendea na kuwafufua. Hapa ameketi mmoja, papa hapa sasa, aliyekufa pale pale ambapo anaketi pale pale. Na yupo hapa angali mzima, usiku wa leo; alianguka kwa ugonjwa mbaya wa moyo. Huyo hapo mke wake, nesi. Tulishuka tukaenda; kila kitu kimetoweka, macho yake yamekaza, na ameaga dunia. Huyu hapa, mzima. "Kwani Yeye aliye *humu* ndani ni mkuu, ndani yetu, kuliko yeye aliye katika dunia!" Unaona?

160 Yeye ni Mkuu! Ni Mungu, Muumba! Pepo na mawimbi ilibidi vimtii Yeye. Pepo walikomeshwa. Maumbile yote yalimtii, kwa sababu Yeye ndiye Muumba wa maumbile. Loo, tunapofikiria hilo, inaondoa maumivu. Basi tunaelewa mambo haya, unaona. Ni nini? Si binadamu. Binadamu hawezi kufanya hivyo; binadamu ni sehemu ya maumbile. Unaona? Lakini ni pepo na mawimbi ambayo humtii Muumba. Unaona?

Na inahitaji Muumba kufanya hivyo, "Kwa maana Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Yeye awezaye kusababisha mchafuko, huyo ndiye aliye katika dunia. Yeye aliyeko ndani yenu, ni Muumba, Ambaye alizifanya pepo. Anaweza kumkemea Ibilisi atoke kwenye pepo, na kuwe kutulivu. Yeye anaweza kumkemea Ibilisi atoke katika tufani, na kusiwe na tufani. Yeye ndiye Muumba. "Na aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia." Unaona?

161 Ibilisi ni wa dunia. Dunia ilikuwa mali yake. Sikuzote imekuwa yake. "Mbona umeanguka, Ewe Lusifa, mwana wa alfajiri?" Unaona, ulimwengu huu ulikuwa ni mali yake. Hapo ni wakati yeye, alipofukuzwa Mbinguni, alirudia duniani. Unaona?

162 Ilikuwa ndiye ambaye alimwambia Kristo, "Milki hizi ni zangu, nazifanyia nipendavyo." Ni zake, na ndiye aliye "katika dunia."

163 Yohana ndiyo kwanza awaambie wanafunzi, "Mmemsikia mpinga Kristo atakayekuja, na tayari yupo hapa akitenda kazi katika wana wa uasi. Lakini, enyi watoto wadogo, ninyi si wa ulimwengu huu. Ninyi ni wa Mungu. Na Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia." Huyo ni Kristo ndani yenu!

164 Yeye ambaye—ambaye aliumba mbingu na dunia, alidhihirishwa katika Utu wa Yesu Kristo; Mungu katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa Nafsi Yake.

Hebu tuseme unasema, "Huyo alikuwa Mwana wa Mungu, basi, Ndugu Branham." Sawa, hebu na tuone kama Yeye ni Mungu asiye na mwisho na wa Milele.

165 Yeye aliyekuwa ndani ya Yoshua alikuwa mkuu, kuliko jua. Na Yoshua alikuwa mtu, aliyezaliwa katika dhambi, kama wewe na mimi. Naye aliyekuwa ndani ya Yoshua na katika jua ambalo lilikuwa likiendelezwa kwa amri ya Mungu alikuwa mkuu. Mungu aliamuru jua liwake na lizunguke, nalo linatawaliwa na kuongozwa kwa amri za Mungu. Lakini Yeye aliyekuwa ndani ya Yoshua alikuwa mkuu, kuliko amri za Mungu; kwa sababu Muumba, Mwenyewe, alikuwa katika Yoshua wakati Yoshua alipolitazama jua na kusema, "Simama hapo ulipo. Nawe, mwezi, wewe ning'inia pale ulipo, mpaka nimalize vita hivi." Na jua na mwezi vikamtii, kwani Yeye aliyekuwa katika Yoshua alikuwa mkuu kuliko ju—jua na mwezi. Yeye aliyekuwa katika Yoshua.

166 Yeye aliyekuwa katika Musa, alikuwa mkuu kuliko Misri. Misri ilikuwa majeshi yenye nguvu sana ya ulimwengu, walikuwa wameushinda ulimwengu wakati ule. Lakini Yeye aliyekuwa ndani ya Musa alikuwa mkuu, kuliko ilivyokuwa Misri, kwa sababu Musa aliishinda Misri. Aliyekuwa ndani ya Musa alikuwa mkuu, kuliko hata maumbile yenyewe. Uliwahi kufikiria kwamba Mungu alichukua Neno Lake akampa Musa, akasema, "Nenda huko ukaamuru kwamba jua lisiwake"? Na jua lilikuwa jeusi kama lami! Hiyo ni kweli? Anaweza kulifanya jua liwake na mawingu yarudi nyuma, au Yeye anaweza kulifanya jua liwe jeusi. Yeye ni Mungu; Yeye anaweza kufanya cho chote atakacho, Naye yumo ndani ya mtoto aaminiye! Amina. Barabara.

167 Hapakuwepo na kiroboto. Pengine ilikuwa msimu wa kipupwe, hakuna nzi, lakini Mungu alimwambia Musa, "Nenda ukanene Maneno Yangu, nami nitaweka kichwani mwako cha kusema. Basi ondoka uende kule ukaokote vumbi ardhini, ukalitupe hewani, hilo vumbi."

168 Ndipo akasema, "Na kuwe na viroboto!" Na viroboto wakawa wanatambaa labda kina cha inchi kadhaa, kila mahali ardhini, mnamo masaa machache. Hiyo ni kweli? Muumba!

169 Hapakuwepo na vyura wo wote, kwa hiyo akanyosha fimbo yake akasema, "Na kuwe na vyura!" Nao wakawepo kila mahali, wamejazana, mpaka nchi yote ilikuwa inanuka. Hiyo ni kweli?

170 Alipofika kwenye Bahari ya Shamu nayo ilikuwa inamzuia, Mungu alisema, "Nena na bahari." Ndipo Musa akanena na bahari; na Yeye aliyekuwa ndani ya Musa alikuwa mkuu, kuliko bahari yenyewe. Hiyo ni kweli? Loo jamani! Sasa, unaona, Yeye aliyekuwa ndani ya Musa alikuwa mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia. Yeye aliyekuwa ndani ya Musa alikuwa mkuu kuliko maumbile yo yote yaliyo katika dunia. Yeye aliyaamuru

maumbile. Kwa lo lote Mungu alilomwambia aseme, alilisema, na hivyo ndivyo ilivyokuwa.

171 Mungu yeye yule yu pamoja nasi usiku wa leo! Siyo tu pamoja nasi, bali ndani yetu! Alithibitisha Yeye alikuwa ndani yetu. "Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia." Tunaogopa nini, dunia?

172 Hapa juzijuzi waligundua a—aina fulani ya jino la dinosa, juu hapa karibu. . . Nadhani ninyi nyote mmesikia habari zake; juu hapa kwenye Maporomoko ya Niagara. Kasema, "Lilikuwa na uzito wa ratili sita." Nilidhani watasema lilitoka kwa mwanadamu, lakini na—nafikiri hatimaye walilifafanua kama namna fulani ya mnyama wa nyakati zilizotangulia kuandikwa kwa historia. Wanyama hao labda waliishi wakati mmoja duniani. Wako wapi sasa?

Je mwajua, Mungu Mwenyezi anaweza kuamuru madinosa kuja duniani humu, katika saa inayofuata wangelundikana maili arobaini? Mnajua, Mungu angeweza kuuharibu ulimwengu huu kwa viroboto? Yeye angeweza kuwaita viroboto. Wanakwenda wapi wanapokufa? Nini kinachowapata inzi? Nini kinachowapata panzi? Msimu wa kipupwe huja, na baridi inashuka kipimo cha arobaini chini ya sifuri; na, ukitoka nje kwenye msimu wa majani kuchanua, panzi wamejaa kila mahali. Walitoka wapi? Yeye ni Muumba ambaye hunena wakawepo! Yeye ni Mungu! Maumbile hulitii Neno Lake.

173 Kitu kinachowavutia wengi wa ndugu zetu, wanapata wazo kwamba Mungu amesema jambo fulani lifanywe, nao wanasema ni BWANA ASEMA HIVI na siyo. Hiyo ndiyo sababu haitukii.

Lakini iwapo ni Mungu kweli anayekwambia, lazima itukie, lazima iwe hivyo. Unaona? Mungu anapolinena, lazima liwe.

174 Yeye aliyekuwa ndani ya Musa ni mkuu, kuliko yeye aliyekuwa Misri. Yeye aliyekuwa katika Musa ni mkuu, kuliko kitu cho chote Farao angeweza kutenda, uchawi wake wote. Yeye aliyekuwa ndani ya Musa alikuwa mkuu, kuliko yeye aliyekuwa katika wale wachawi. Unaona? Yeye aliyekuwa ndani ya Musa ni mkuu, kuliko maumbile yote.

175 Mkuu zaidi! Yeye aliyekuwa ndani ya Danieli alikuwa mkuu kuliko wale simba. Yeye aliweza kuwazuia hao simba wenye njaa. Kwa hiyo kitu cho chote kinachoweza kuzuia cho chote, ni kikuu kuliko kile yeye alichozuia. Kwa hiyo simba wakatoka mbio, wenye njaa, wamle Danieli; Naye aliyekuwa ndani ya Danieli alikuwa mkuu, kuliko yeye aliyekuwa katika hao simba.

176 Sasa, wakati simba alipoumbwa kwanza, alikuwa rafiki wa binadamu. Ni Ibilisi anayemfanya yeye afanye hayo. Hiyo ni kweli. Katika ule Utawala wa Miaka Elfu, mbwa mwitu na mwanakondoo watakula pamoja, na simba atakula majani kama fahali, nao watalala pamoja na fahali. Hawatadhuru wala kuharibu katika ule Utawala wa Miaka Elfu. Ibilisi atakuwa

ametoweka. Ibilisi ndiye anayewafanya wanyama wa mwituni waharibu na kurarua na kula, na mambo kama hayo, jinsi wafanyavyo. Ni Shetani anayefanya hivyo. Bali Yeye aliyekuwa ndani ya Danieli alikuwa mkuu, kuliko yeye aliyekuwa katika simba. Unaona? Yeye alikuwa mkuu ndani ya yule nabii, kuliko yeye aliyekuwa katika simba.

177 Yeye aliyekuwa katika wale wana wa Kiebrania alikuwa mkuu, Yeye aliyekuwa ndani yao alikuwa mkuu, kuliko yeye aliyekuwa katika ule moto. Kwani walitupwa motoni; na Yeye aliyekuwa ndani yao, alikuwa pamoja nao, na akauzuia moto usiwaunguze wakati ile tanuru ilipotiwa moto 'mara saba kuliko ilivyowahi kutiwa,' kutiwa moto. Hiyo ni kweli? Yeye aliyekuwa pamoja na wana wa Kiebrania alikuwa mkuu, kuliko yeye aliyekuwa katika dunia.

178 Hapo aliketi Nebukadreza, au Belshaza. Nebukadreza, naamini ndiye, aliyeamuru tanuru itiwe moto mara saba kuliko ilivyopata kutiwa. Amevuviwa na Ibilisi, kuwachukua watu hawa, kwa sababu walikuwa wanalitetea Neno la Mungu; na akawatupa kwenye tanuru hii, imetiwa moto mara saba kuliko ilivyopata kutiwa, na hata haikuweza kuwaunguza. Kwani Yeye aliyekuwa pamoja na Shadraka, Meshaki na Abednego, alikuwa mkuu, kuliko yeye aliyekuwa katika dunia. Bila shaka! Loo, jamani!

179 Yeye aliyekuwa ndani ya Eliya alikuwa mkuu, kuliko zilivyokuwa zile mbingu za shaba, sababu aliweza kuleta mvua kutoka kwenye mbingu za shaba ambazo hazikunyesha mvua kwa miaka mitatu na miezi sita.

Yeye aliyekuwa ndani ya Eliya ni mkuu, kuliko mauti. Kwani, ulipotimia wakati wake wa kufa, Mungu alimwona huyo nabii, mzee aliyechoka. Alikuwa akimkemea Yezebeli na vipodozi vyake vyote na mambo ya kisasa, naye alikuwa kwa namna fulani amechoka, kwa hiyo Yeye hata hakumwacha aende nyumbani kwa kutwaliwa, kama Yeye alivyomfanyia Henoko. Alipeleka gari likamchukua juu, likampeleka Nyumbani. Yeye aliyekuwa ndani ya Eliya ni mkuu, kuliko yeye aliyekuwa katika Yerusalemu na Yuda, na milimani. Yeye alikuwa mkuu katika Eliya, kuliko mauti yenyewe. Yeye aliyekuwa ndani ya Eliya ni mkuu, kuliko kaburi; sababu aliepuka kaburi, aliepuka mauti, naye akapanda tu kwenda Nyumbani katika gari. Unaona, Yeye alikuwa mkuu, Naye alikuwa ndani ya Eliya.

180 Unasema, "Loo, vema, huyo alikuwa mtu mkuu."

181 Ngoja kidogo! Biblia ilisema, "Yeye alikuwa mtu wa tabia moja na sisi," kama mimi na wewe. Hiyo ni kweli. Lakini alipoomba, aliamini amepata alichoomba; Yesu alivyotuambia, "Mnapoomba, amininі ya kwamba mnayapokea mnayoyaomba, yatatendeka." Aliomba kwa bidii kwamba isinyeshe, na

haikunyesha kwa miaka mitatu na miezi sita. Unaona? Yeye aliyekuwa ndani ya Eliya alikuwa mkuu, kuliko maumbile.

182 Basi vipi kuhusu kuponya wagonjwa? Unaona? Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko maradhi. Unaona? Kwa sababu, huko ni kukatizwa, kukatiza sheria za Mungu hasa, maradhi ni katizo. Vema, aliye mkuu ni Yeye aliye ndani yako, huyo ni Mponya na Muumba, kuliko yule—kuliko Ibilisi aliyekatiza mpango halisi wa maisha yako. "Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia." Unaona?

Yeye aliyekuwa ndani ya Eliya alikuwa mkuu! Yeye aliyekuwa ndani ya Isaya ni mkuu, kuliko wakati ulivyokuwa; au ye yote wa wale manabii, kwa sababu waliona ng'ambo ya wakati. Unaona?

183 Yeye aliyekuwa ndani ya Ayubu ni mkuu, kuliko hata mabuu, na mauti na kaburi. Kwa sababu, kwa ono aliona kuja kwa Bwana, naye akasema, "Mkombozi wangu yu hai, na hatimaye Yeye atasimama juu ya nchi; na ingawa hata baada ya mabuu yangu ya ngozi kuuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu." Unaona? Yeye aliyekuwa ndani ya Ayubu ni mkuu, kuliko mauti; mkuu zaidi, sababu mauti ilijaribu kumchukua ikashindwa. Haikuweza kufanya hivyo, kwa sababu alisema, "Nitafufuka tena," naye alifufuka. Alifufuka.

184 Sikiliza, laiti tungekuwa na wakati wa kuendeleza jambo hili. Lakini ningetaka kuuliza swali, ambalo nimelisikia likitajwa majuzi, kuhusu, "Kristo ndani yenu," [Ndugu Branham anagonga mara mbili mimbarani.]

Sasa, usi—usiiache itegemee kitu ambacho umetenda; useme, "Nilisikia msisimko mdogo. Ni—ni—nilinena kwa lugha. Ni—nilicheza katika roho." Sina neno dhidi ya jambo hilo, sasa. Hilo ni sawa, unaona, hilo ni, lakini usitegemee jambo hilo. Unaona?

Maisha yako yabidi kuwa *Hili*. [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake—Mh.] *Hii* Ndiyo. Wewe na *Hii* yabidi muwe mmoja, unaona, halafu *Hili* hujidhihirisha Lenyewe. Unaona?

185 Sasa vipi kama—vipi kama usiku wa leo ungeweza kusema, kwa moyo wako wote, kwamba roho ya Shakespeare iliishi ndani yako, kwamba Shakespeare aliishi ndani yako? Unajua ambacho ungetenda? Ungetenda kazi za Shakespeare. Ungezitenda. Ungezitenda. Ungetunga mashairi na—na michezo ya kuigiza, na kadhalika, kwa sababu Shakespeare alikuwa msanii wa namna hiyo, mwandishi maarufu, mshairi. Sasa, kama Shakespeare angeishi ndani yako, kazi za Shakespeare ungezitenda. Sivyo?

186 Vipi kama Beethoven aliishi ndani yako? Vipi kama Beethoven aliishi ndani yako? Unajua ungefanya nini? Ungeandika nyimbo kama Beethoven, yule mtunzi maarufu. Ungeandika nyimbo kama Beethoven, kwa sababu Beethoven

angekuwa uhai wako. Ungekuwa Beethoven, aliyefanyika mwili, tena. Kama Beethoven aliishi ndani yako, ungetenda kazi za Beethoven, sababu Beethoven aliishi ndani yako. Sivyo?

187 Bali Yeye aliye ndani yako ni Kristo! Na kama Kristo yu ndani yako, kazi za Kristo utazitenda, kama Kristo anaishi ndani yako. Yeye alisema hivyo. Yohana Mtakatifu 14:12. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizitendazo Mimi yeye naye atazitenda," kama ulikuwa ndani ya Kristo, au kama Kristo aliishi ndani yako. Basi, Kristo ni Neno. Sivyo? Nalo Neno huwajia manabii Wake. Unaona? Na kama, wewe, Kristo aliishi ndani yako, kazi za Kristo zingetendeka kupitia kwako, Maisha ya Kristo yangeonekana kwako. Kazi alizozifanya Yeye, maisha aliyoishi Yeye, na kila kitu, kingeishi ndani yako; kama tu Shakespeare, au Beethoven, au—au ye yote aliishi ndani yako.

188 Kama Uhai Wake! Lakini kama bado unaishi maisha yako mwenyewe, basi utafanya kazi zako mwenyewe. Unaona? Lakini kama unaishi Maisha ya Kristo, kama Kristo yuko ndani yako, "Yeye aliye ndani yako ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Kama mashaka yako na wasiwasi kuhusu ahadi ya Mungu viko ndani yako, basi Kristo hayuko mle; unaona, umejifanya tu. Lakini kama ule Uhai, kama Kristo anaishi ndani yako, Neno Lake Yeye atalitambua na ahadi Yake Yeye atatenda. Unaona? Atatenda.

189 "Unapoomba, amini kwamba unapokea unachoomba, nawe utapewa. Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' nawe usitie shaka moyoni mwako, lakini uamini kwamba lile unalosema litatukia, litakuwa lako. Baba anatenda kazi, nami ninatenda hata sasa. Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe; ila yale anayoona Baba akitenda, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile." Unaona? Na wakati Baba alipomwonyesha Yeye la kutenda, alikwenda kule bila ya kushindwa na cho chote, na kasema, "Iwe," ikawa.

Na Kristo yeye yule anaishi ndani yako. Anaishi ndani yetu. Basi kazi Zake tutazitenda, kwa sababu Kristo ni Neno, na ahadi ya Neno husababisha kuponywa kwako. Unaamini hayo? [Kusanyiko linasema, "Amina"—Mh.] Hakika!

190 Yeye alisema, "Sitawaacha ninyi yatima." Ninapoomba, niliuliza muda mfupi uliopita, hapo katika Mathayo 24, unaona, au Mathayo 28:20. Unaona? Yeye alisema, "Naja kwenu, niwe ndani yenu. Mimi," ule Utu, Kristo, katika hali ya Roho Mtakatifu, "nitakuja na kuishi ndani yenu. Ndipo hamtakuwa—hamtakuwa ninyi wenyewe tena. Nitakuwa ndani yenu. Na Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia." Unaona? Waebrania 13:8 inasema, "Ni yeye yule, jana na hata milele."

191 Yeye aliyekuwa katika Nuhu alikuwa mkuu kuliko hukumu za maji.

Na Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko hukumu za moto. Unaona? Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kwa sababu Yeye aliilipia ile hukumu na akaishinda Hukumu kwa ajili yenu. Unaona? Hakuna hofu kwa jambo hilo. Unaona, mumo mle ndani. Ndiyo.

Yeye aliyekuwa ndani ya Nuhu ni mkuu, kuliko yeye aliyekuwa katika hukumu za maji, zilizouharibu ulimwengu ambao haukuamini. Kwa sababu, Nuhu aliamini. Naye aliyekuwa ndani yake ambaye alimwamini aliyenena naye, ni mkuu kuliko yeye aliyekuwa katika dunia. Kwamba, Nuhu aliepuka hukumu yote, kwa sababu Neno la Mungu lilikuwa kuu kuliko hiyo, naye akaelea juu ya hizo hukumu.

"Mkuu zaidi!" Jinsi tungeweza kushikilia hilo kwa muda mfupi! Unaona?

192 Yeye aliyekuwa ndani ya Daudi ni mkuu, kuliko dubu aliyeiba kondoo wake. Yeye aliyekuwa ndani ya Daudi ni mkuu, kuliko simba aliyewavamia na kuchukua mmoja wa wanakondoo wake. Yeye aliyekuwa ndani ya Daudi ni mkuu, kuliko yule adui, Goliathi. Lile pandikizi la Kifilisti lililosimama pale, lapata urefu wa futi kumi na mbili, kumi na nne, lenye vidole vya inchi kumi na nne; na mkuki kama sindano ya mfumaji; na limefunikwa kila mahali kwa shaba nyeupe, chuma cha pua au madini chenye unene wa inchi mbili au tatu. Lakini aliyekuwa ndani ya Daudi alikuwa mkuu kuliko kilichokuwa ndani yake.

Alikuwa nguvu, misuli. Alikuwa shujaa wa vita. Aliweza, alisema tu angemwokota Daudi kwa ncha ya mkuki wake na kumning'iniza juu, na kumwacha aliwe na ndege.

193 Ndipo Daudi akasema, "Unanikabili mimi kama Mfilisti, katika jina la Mfilisti. Unanilaani katika jina la mungu wa Kifilisti." Akasema, "Umejisifia utakalotenda. Nawe unanijia kwa silaha na mkuki. Lakini nakujia katika Jina la Bwana Mungu, na siku ya leo nitakiondoa kichwa chako kwenye mabega yako." Naye akafanya hivyo, kwa sababu Yeye aliyekuwa anamvuvia Daudi apate ushupavu huo ni mkuu.

194 Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko hicho kiti cha magurundumu. Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko machela hayo. Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko kansa hiyo. Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko mateso hayo. Yeye ni mkuu, kuliko kitu cho chote kilichopo ambacho Ibilisi angeweza kukuwekelea. "Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia." Yeye ni mkuu zaidi! Ndiyo!

Daudi alikuwa mkuu, kilichokuwa ndani ya Daudi; Mungu ndani ya Daudi.

195 Yeye yu ndani yetu, yaani, Kristo. Yeye alikuwa mshindi wa kila adui, kwa ajili yetu. Wakati Yeye alikuwa hapa duniani, alishinda dhambi, akashinda maradhi, akashinda mauti, akashinda kuzimu, akashinda kaburi, na sasa Yeye

yuaishi ndani yetu kama mshindi! Yeye alishinda maradhi, kuzimu, mauti, kaburi, na akaja kwetu kutuweka huru na mambo hayo yote. Na Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko yeye ambaye anaweza kuweka madanganyo haya juu yako. Ndiyo! "Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia."

196 Hivyo ndivyo miujiza hii inavyotendeka. Hivyo ndivyo upepo ule ulivyokoma, juzijuzi. Je! binadamu angeweza kufanya hivyo? La, bwana, haiwezekani. Niliposimama pale, nikilia, na hayo mawimbi yakivumisha, na . . .

Wangapi ndani humu, walikuwepo kule juu? Hebu tuone mkiinua mikono yenu. Inueni mikono yenu, kila mmoja aliyekuwa kule juu, huko Calorado wakati—wakati ule. Sawa. Ndugu Fred, nadhani, ndiye tu aliyekuwepo, wakati huo. Nilifikiria labda Ndugu Mann alikuwepo hapa, lakini yeye . . . Ndugu, Ndugu Evans, sivyo? Ndugu Evans alikuwepo juu kule wakati ule. Ndiyo. Sawa. Na, ndiyo.

197 Angalia. Je! hiyo si kweli? Je! hivyo sivyo ilivyotendeka? Mvua zikakoma, na pepo zikakoma kuvuma. Ilikuwa nini? Kwa neno langu? La! Kwa sababu Yeye aliniambia nifanye hivyo. Na Yeye aliye ndani yetu ni mkuu, kuliko maumbile yo yote. Je! huyo si Mungu yeye yule ambaye aliweza kutuliza mawimbi baharini, kuzifanya pepo zirudi makwao? Je! Yeye si yeye yule Ambaye angeweza kulitia jua giza, angeweza kulifanya jua liwake? Vema, "Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia." Unaona? Vema.

198 Sasa hiyo ndiyo maana miujiza hii ya kweli inaweza kufanywa, kwa sababu ni ahadi ya Mungu. "Mambo nitendayo Mimi, ninyi nanyi mtayatenda." Yohana Mtakatifu 14:12. Yeye, Kristo, ambaye alizituliza zile pepo na mawimbi, Ndiye Muumba wa hayo. Yeye bado ni Muumba kama Yeye alivyokuwa wakati huo. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Yeye aliwaponya wagonjwa na akaiharibu dhambi, na akabadilisha yote kwa ajili yako, naye akaja kwako kusudi Yeye apate kuishi pamoja nawe. Yeye alishinda yote haya, kusudi aje akaishi ndani yetu. Yeye Ndiye yule Mshindi ambaye tayari ameshinda mambo haya; aliyathibitisha katika Maandiko, akarudi akashinda kila kitu, na kuwathibitishieni kwamba Yeye ni Mungu yeye yule. Na baada ya miaka elfu moja mia tisa, [Ndugu Branham anagonga mara tano kwenye mimbara—Mh.] Huyu hapa angali anatenda jambo lile lile miongoni mwetu alilotenda Yeye wakati huo, ambaye ayashinda mauti, kuzimu, maradhi, na kaburi!

199 Huyu Kristo, Huyu "Yeye," Yeye Ndiye aliye ndani yako. Yeye ni Kristo. Kama Yohana alivyosema, "Yeye aliye ndani yako ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Huyo alikuwa Kristo! Yeye ni mkuu kuliko ulimwengu wote kwa sababu Yeye aliushinda ulimwengu, naye ni mkuu, kuliko mambo yote hayo,

kwa sababu Yeye aliyashinda kwa ajili yetu. "Nasi tu zaidi ya washindi kwa Yeye ambaye alitupenda na kujitoa Mwenyewe kwa ajili yetu," kusudi apate kurudi na kutenda kazi Zake kwa kupitia sisi, kututhibitishia kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Wakati Yeye alipokuwepo duniani, alithibitisha aliposimama miongoni mwa watu, kwamba Yeye alikuwa Masihi. Aliweza kutambua mawazo yaliyokuwa ndani ya mioyo yao. Na Biblia ilisema, Musa alisema, kwamba, "Yeye angekuwa nabii." Sivyo? Yeye alijua siri za mioyo. Yeye alijua watu wale walikuwa ni akina nani. Yeye alijua wana shida gani. Je! tumeona hilo likitendeka? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Wakati baada ya wakati!

200 Tunajua kwamba wafu wamefufuliwa, moja kwa moja katika mauti. Baadhi yao walikuwa wamekufa kwa siku moja na nusu. Vema, akafa asubuhi moja, nao wakamrudisha usiku ule, na wakasafiri usiku mzima; na adhuhuri ya siku iliyofuata, au muda kidogo baada ya saa sita, akaletwa kwenye hema. Mtoto mchanga aliyekufa, baridi, na amewekwa mikononi mwa mama yake. Ndipo Bwana Mungu akamleta, akanena Neno la Uzima, na mtoto huyo akapata joto na akaanza kulia; kamrudisha mikononi mwa mama yake.

201 Bibi Stadklev, amesimama pale akiona hilo likitendeka, hiyo ndiyo sababu alilia hivyo kwa ajili ya mtoto wake, alinitaka mimi niruke kwenda Ujerumani. Lakini Bwana akasema, "Huo ni mkono Wangu; usikemee jambo hilo." Unaona, unajua la kufanya.

Wakati Yeye alipomwambia Musa, akasema, "Uambie mwamba," usiupige. Hiyo ilimaanisha "uambie," usiupige, unaona. Yakubidi kutii analosema utende. "Lakini hakuna mtu anayeweza kufanya cho chote yeye mwenyewe," yambidi asikie kwanza kutoka kwa Mungu.

202 Sasa Neno la Mungu liliahidi kwamba Yeye yu hai. Na, kwa kuwa Yeye yu hai, wewe u hai. Yeye aliahidi, kwamba, "Kazi nizifanyazo Mimi nyinyi nanyi mtazifanya. Mambo yale yale, ila mengi zaidi, mtayatenda, kwa sababu naenda kwa Baba." Yeye alishinda vitu vyote. Yeye Ndiye aliyetuliza . . .

Yeye Ndiye aliyewafanya wale kindi. Hilo lilitukia mara mbili. Lilitukia mara moja chini kule kwako, Charlie. Na ilitukia—ilitukia juu hapa wakati, ndugu, Ndugu Fred na Ndugu Banks na hao wengine juu kule pamoja nasi.

203 Limetukia kule Ujerumani, wakati hao wachawi kumi na watano, wamenizunguka pande zote, wakasema . . . Kwa sababu Billy na Ndugu Arganbright wasingewaruhusu—wasingewaruhusu wanione mimi, ndipo akasema, "Vema, tutasababisha hema hilo lipeperushwe na upepo." Nao wakaketi hapo chini, huku wananuiza uchawi wao, na kuita mungu wao,

Ibilisi, na huyu hapa anashuka kwa tufani. Yapata Wajerumani thelathini elfu, arobaini elfu nje kule, na hema lile likiinuka tu juu na chini *hivi*.

Wao, ndipo wakakata, walichukua makasi wakakata unyoya, na kuuelekeza nyuma namna *hiyo*. Na kusema yao, wakinuiza uchawi wote, na kusema yale maneno matatu matakatifu wanayosema, "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; lu—lu—lu—lu—lu—lu! Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; lu—lu—lu"

204 Wakiendelea namna hiyo, na kwa kweli tufani ikaja. Hakika. "Yeye ni mfalme wa uwezo wa anga," Shetani. Nao wakaita tufani. Na, sasa, hata hema lile kubwa mno likikaa namna hiyo, loo jamani, lingefunika umbali wa jengo moja la mji; nalo lilijenga, lilijengwa na mbili kwa nne-nne, na turubai limefungwa juu yake. Upepo ukaingia chini kule na kuliinua tu, namna *hiyo*. Na upepo ule, na umeme ukimulika hivyo, niliendelea tu kuhubiri.

205 Na, loo, walikuwa wakiingia kwenye mnuizo mkubwa, wakiendelea na kuendelea namna hiyo, wakitamka maneno hayo madogo matakatifu waliyosema, "Yale maneno matatu makuu na matakatifu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," pande zote mbili namna hiyo. Ndipo nikamwona akisujudu, na amezungukwa na pepo pale, lakini hawakufungwa.

206 Nami nikamwambia Ndugu Lowster, "Usifasiri haya."

207 Nikasema, "Ndugu Arganbright, omba tu."

208 Nikasema, "Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, Wewe ulinituma hapa. Nimeweka mguu wangu kwenye ardhi hii ya Ujerumani, katika Jina la Yesu Kristo, kwa sababu Wewe ulinituma hapa. Na wingu lile halina mamlaka juu yangu. Halina, kwa sababu nimepakwa mafuta na kutumwa hapa kwa ajili ya wokovu wa watu hawa."

"Nakuamuru, katika Jina la Yesu, uondoke hapa."

209 Na ngurumo, zikenda, "Bang'! Bang'! Bang'!"—zikafanya "ngrrrrrrrrr," na kuondoka, na moja kwa moja juu ya hema, zikavuma zikitoweka; kisha jua likawaka.

210 Katika dakika kumi, kulikuwa na kama kumi elfu kwenye madhabahu na sehemu nyingine, wakililia rehema, kwa kuona uwezo wa Mungu. Kwa nini? "Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia." Unaona?

211 "Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko yeye aliye duniani." Unaona mateso yale katika jambo lile, loo, ndugu, dada, hatuna wasiwasi hata mmoja kamwe. Ukuu ni Mungu, na Yeye yuko ndani yenu. Mnaamini hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

212 Sasa nimepitisha muda sana. Ni kama tu dakika kumi na tano, baada ya saa tatu. Nami najua watu hawa wana safari ndefu ya magari.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kidogo.

213 Ee Baba Mungu, Wewe unajua kuhusu Colorado. Unajua mambo hayo ni kweli. Nami nalinena kwa ajili ya utukufu Wako, kusudi watu hawa wapate kujua. Baada ya uthibitisho wote wa kisayansi, wa zile picha, na kazi za Roho Mtakatifu. Na, Bwana, Wewe unajua kwamba Yeye. . . nilitaja waziwazi kwa watu, na sikuzote mimi hufanya hivyo, kwamba ni kwa sababu Wewe uliahidi hilo. Na Wewe uko hapa, ukijaribu kumpata mtu fulani ambaye Wewe unaweza kujithibitisha Mwenyewe kupitia kwake, kuwafanya wengine waone kwamba Wewe u hai, na Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninakuomba Wewe, Bwana, uturehemu, na utuelekeze na kutuongoza katika mawazo yetu.

214 Kuna wale wanaoketi hapa ambao ni wagonjwa na wanateseka. Kuna wale ambao labda huenda wakafa kama hawapati msaada toka Kwako. Wengi wao, labda, wamefikia mwisho wa safari yao, ambapo madaktari hawawezi tena kuwasaidia. Wewe ni Mungu, na Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na Uwepo Wako upo hapa.

215 pia, Bwana, hatujui vile huu Mvuto wa Tatu, kama tulivyoutaja Huo, utakavyokuwa. Sijui ni nini. Lakini tunajua jambo moja, kwamba Mvuto wa Kwanza ulikuwa utimilifu. Mvuto wa Pili, ukiwa wa tano, ulikuwa neema.

Na, Mungu, naomba usiku wa leo kwamba Wewe utajifunua Mwenyewe kwetu, kwamba baada ya mambo haya, kusema, "Yeye aliye ndani yenu!" Nawe ulisema, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya," na ulisema Wewe hukutenda kitu mpaka Baba alipokuonyesha Wewe.

216 Nasi tumeona ambalo Wewe ulitenda wakati ulipoweza kumwambia Mtume Petro jina lake ni nani, jina la baba yake ni nani. Kamwambia Nathanieli utume wake ulikuwa nini, jinsi yeye alivyokuja pale, alikokuwa hapo kabla, alichotenda. Kamwambia yule mwanamke, kisimani, kuhusu dhambi zake na jina lake, akiishi katika huu uzinzi na hawa wanaume sita; watano alikwisha kuwa nao, na yule aliyekuwa anaishi naye sasa hakuwa mumewe. Wewe bado u Mungu yeye yule. Ulimwambia . . .

217 Ilikuwa hali ya upofu wa Bartimayo, huku amesimama pale; lakini hata hivyo, moyoni mwake, ameona maono, kwamba yeye angeweza kuona; kwamba, kama huyo alikuwa Yehova aliyedhihirishwa katika Uwana wa Yesu Kristo, kwamba Yeye aliweza kujua kilio chake. Basi akapaza sauti, "Ee Mwana wa Daudi, unirehemu!" Nayo ikakusimamisha Wewe, Nawe ukageuka ukamponya, Ee Baba, ukimwambia yeye imani yake imemwokoa.

218 Maskini yule mwanamke aliyepungukiwa na damu, ambaye kwa kutokwa huku na damu na badiliko la maisha, na

kwa miaka mingi haikukoma. Alikuwa ametumia fedha zake zote kwa madaktari, na hakuna hata mmoja wao angeweza kumsaidia. Alikuja kwenye mmoja wa mikutano Yako wakati Wewe ulipokuwa unamzungumzia mtu huko—huko Galilaya, wakati Wewe ulipokuwa njiani ukienda kwa Yairo. Maskini mwanamke huyu alikuwa amesema moyoni mwake, bila ya Andiko nyuma yake, "Kama nikiweza tu kugusa vazi Lake, na—naamini kwamba nitakuwa mzima." Naye akapata haja yake wakati alipogusa vazi Lako. Nawe ukamwambia yeye kwamba imani yake imetenda jambo hilo, ukasimulia haja zake, naye akaponywa.

219 Tunaambiwa katika Neno kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu, uketiye huko Juu, uishiye sikuzote kufanya upatanisho. Na—na pia kwamba Wewe, ukiwa Kuhani Mkuu, wakati huu, ambaye anaweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu. Bwana Mungu, jalia kwamba kila mtu hapa usiku wa leo aweze. . . awe na majaliwa ya kukugusa Wewe usiku wa leo, yule Kuhani Mkuu sana, na apate afya. Kwa Utukufu wa Mungu, naliomba katika Jina la Yesu. Amina.

220 Sasa si. . . Kuna kadi za maombi? Ni—nilimwambia Billy asi. . . kuna mtu aliye na kadi za maombi? Sawa, hiyo ni sawa, nilimwambia asizitoe. Nilifikiria pengine ningechukua muda mrefu kidogo, wakati mimi. . . loo, ninazungumza sana. Bali, angalia, unaona, na mliniambia, niliposema, "Nitajaribu kutoka kwenye saa mbili na nusu," mlicheka, nami ni—nilijua mlijua mlilokuwa mkizungumzia. Mi—mimi ni. . . lakini na—nawapenda. Unaona?

221 Ni, ninalojaribu kufanya, sikuzote nimejaribu jambo hili, rafiki; si kwa mtu ye yote kusema, "Ndugu Branham alifanya jambo hili." Ndugu Branham hawezi kutenda kitu. Unaona? Ni Yesu Kristo. Na Yeye aliye ndani yangu yuko ndani yako. Yakubidi tu kuamini. Sivyo? Unaona? Yeye aliye ndani yako ni mkuu kuliko ugonjwa wako.

222 Sasa ni watu wangapi humu ndani ambao ni wagonjwa miilini mwao, hawanijui mimi, lakini unaamini kwamba una imani ya kutosha kumgusa Kuhani Mkuu, inua mkono wako, useme, "Ninaamini hilo"? Sawa. Loo, kuna mikono, karibu kila mahali. Sawa. Wangapi humu ndani wananijua mimi, na wanajua sijui cho chote kuhusu unachohitaji, nawe unataka Mungu akuguse? Inua mkono wako. Unaona? Unaona? Sawa.

223 Kwa kweli, hakuna mtu humu ndani ambaye ninajua cho chote kumhusu, wakati huu wa sasa, kuhusu kuwa mgonjwa. Lakini mvulana huyu anayeketi hapa, namjua. Nimemwombea, mara nyingi. Sikumbuki jina lake, lakini anatoka huko Kentucky. Ananiandikia barua wakati wote, rafiki msiri wa Ndugu na Dada Woods na hao wengine, naye huja pale. Naye

amehudhuria mikutano kwa muda mrefu, mrefu sana. Huyo ndiye mtu pekee ambaye namjua.

224 Sasa, Ndugu Dauch, kadiri ninavyojua, ni mzima, la sivyo asingekuwa ameketi hapa. Yeye alikuwa mgonjwa sana juzijuzi, na Bwana akamponya.

225 Simjui mtu *huyu*. Na sijui ni nani aliye na mikongojo hii hapa; pengine ni ya mtu yule kitini pale. Si—sijui.

Nami na—nawajua wengi wenu. Lakini Mungu Mbinguni anajua, wakati huu, sijui mnachotaka. Sina habari. Kwa namna fulani ni vigumu hapa Maskanini, sababu, unaona, nawajua watu wengi sana.

226 Sasa hivi ndivyo ilivyo. Unapofikia mahali . . . Sasa, ninakuja hapa, wakati mwingine, na nikasema, "Sawa, tutampa kila mtu kadi ya maombi na kuwapanga mstari. Njoni hapa jukwaani." Mtu fulani atakwenda zake . . . Sasa huwezi . . .

Sasa, marafiki, nitaufungua moyo wangu na kuwaambieni jambo fulani. Huwezi kulificha hilo. Lile unalowaza tu, nalijua. Hiyo ni kweli. Najua unalowazia. Unaona? Na wakati mwingine unasema, "Ndugu, ninaamini." Mbona, vema, unaamini kwa kiasi. Unaona? Unaona? Ninajua.

227 Na papa hapa, vema, sasa, sasa hivi tu, upako unanijia sasa hivi, unaona. Na ninaweza kuhisi tu mapigo yale, kama, kutweta, unaona, kupigapiga kutoka sehemu mbalimbali. Unaona?

Bali sasa usi—usikose tena kuamini. Amini Ujumbe wote. Uamini Huo. Kama siyo, kama haukuandikwa katika Biblia, basi usivamini. Lakini kama Huo umo katika Biblia, basi Roho Mtakatifu ambaye anaishi ndani yetu anawajibika kutekeleza jambo Hilo kama tunaliamini. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Najua ni vigumu. Unaona, hakuna kinachokuja kwa urahisi.

228 Ilikuwa vigumu Kwake Yeye kufa, ili hili liweze kuletwa kwenu. Ilikuwa vigumu Kwake Yeye kwenda Kalvari; Yeye alitaka kukaa, kiasi kwamba hata Yeye alilia, "Si mapenzi Yangu, bali Yako yatendeke." Unaona? Unaona? Yeye hataki kuondoka; Yeye alikuwa Kijana, Naye, alikuwa na ndugu Zake. Aliwapenda kama tu ninavyowapenda ninyi. Lakini Yeye—Yeye hangeweza kuishi, na wao waishi pia, kwa hiyo Yeye alikufa tupate kuishi. Hilo halikuwa jambo rahisi. Ilimbidi alitende. Tazama ni mauti ya namna gani iliyokuwa mbele Yake, "Baba, saa imefika, Nami je! niombe kwamba Wewe uniondolee Mimi kikombe hiki? La." Yeye hakutaka kufanya hivyo; Yeye alitaka mapenzi ya Mungu yafanyike.

229 Sasa, tazama, kama utaamini jambo lilo hilo! Sasa, usi—usi—usilitilie shaka Hilo, kamwe. Hebu liamini tu hilo. [Ndugu Branham anagonga mara kadha mimbarani—Mh.] Liamini kabisa. Usitie shaka. Liamini tu.

230 Kama nikiwaleta watu kweye mstari wa maombi, na niseme, "Vema, sasa mtu huyu, unajua sikujui."

231 "La, hilo ni sawa, Ndugu Branham."

232 Ndipo pindi kule nje utampata mtu fulani akisema, "Ah—aha, lakini yeye anasoma walichoandika kwenye kadi ile ya maombi! Ni kusoma mawazo!" Kwa kweli kutafaulu tu.

233 Halafu nitasema, "Vema, sasa Jumapili hii hatutatoa kadi zo zote za maombi. Nataka kila mtu hapa, ambaye ni mgeni, hawajawahi kuwepo hapa hapo kabla, asimame." Unaona? Na—na halafu Roho Mtakatifu atageuka moja kwa moja na kutambua yote yaliyokuwa ndani yao. Unaona? Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaliona pande zote mbili.

234 "Loo, vema, kuna kasoro kwenye jambo hilo." Unaona? Unaona? Hapo, hakuna njia, hu—hu—huwezi . . . Unaona, maadamu Shetani anaweza kupata nafasi, atakufanya tu wewe uamini cho chote kile.

Naye atakuonyesha kila kosa nililo nalo, na ninayo mengi sana anayoweza kukuonyesha. Lakini usiyaangalie hayo! Usiangalie hayo. Mimi ni mtu. Unaona? Lakini, kumbuka, Neno hili la Mungu ni Kweli, nami ninajaribu kuishi Kwalo.

235 Kama nikitoka niende hapa nje na kuanza kutenda mambo mabaya, ambayo si sahihi, kutenda dhambi, na kunywa pombe, na, au kuvuta sigara, au—au kufanya mambo ambayo hayafai, wewe—wewe njoo uniketishe chini, sababu hilo—hilo halifai. Na—nataka basi kuondoka ulimwenguni. Si . . . Nataka kuondoka kabla hayo hayajatukia. Unaona? Sitaki kufanya hivyo.

236 Lakini maadamu ninajaribu kuishi sawa na kutenda lililo sawa, unaona, na kujaribu kuishi kama impasavyo Mkristo, na halafu kuacha Mungu achukue Neno Lake na kunisikia mimi nikilitetea Hilo. Ingawa Hilo litanigharimu marafiki wengi na kupendwa na ulimwengu, na mambo kama hayo, na kuchukiwa na wengi, na madhehebu, wananifukuza, hata hivyo nataka kuwa mwaminifu kwa Neno hili. Ni Neno la Mungu, nami nampenda Mungu. Kwa hiyo ni Neno la Mungu, nami—nami nawaambia kwamba, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele," na Yeye yuko ndani yetu sasa. Na kama u . . .

237 Sasa, kama uhai wa Shakespeare ulikuwa ndani yangu, ukiishi ndani yangu, kama Shakespeare aliishi ndani yangu, si ningetenda kazi za Shakespeare? Kama Beethoven yu ndani yangu, si ningetenda kazi za Beethoven? Kama roho ya Dillinger ilikuwa ndani yangu, kama John Dillinger angeishi ndani yangu, si ningekuwa John Dillinger mwingine? Kama Beethoven angekuwa ndani yangu, je! ningekuwa Beethoven mwingine? Unaona? Kama Castro alikuwa ndani yangu, je! ningekuwa Castro mwingine? Unaona?

Na kama Yesu Kristo yu ndani yangu, kazi Zake nitazitenda, kwa sababu ni Yeye. Na je! hakusema kwamba jambo lile lile lingelitendeka? Unaona? [Kusanyiko linasema, "Amina"—Mh.]

238 Sasa Yeye angefanya nini kama angekuwa anasimama hapa, kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Yeye angesema, "Naweza kufanya tu ambalo Baba hunionyesha nitende." Sivyo? Vema, hivyo ndivyo Yeye alivyotenda jana.

Sasa Yeye ni yeye yule? Na maradhi je? Gharama yako imekwisha lipiwa. Kila mmoja wenu tayari amekwisha kuponywa ugonjwa wake. Sivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa maana hilo...Kila mmoja wenu amesamehewa, bali yakubidi uukubali. Kila mmoja wenu ameponywa, lakini yakubidi uukubali.

239 Sasa, kuthibitisha kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kama Yeye angekuwa anasimama hapa, Yeye hangeweza kukuponya, kamwe, na kutoamini kwako. Ingelikubidi kuamini, vile vile tu kama ingekubidi kuamini hilo sasa hivi. Itabidi iwe vile vile, unaona. "Sababu, kazi nyingi kuu Yeye hakuweza kutenda katika siku Zake, kwa sababu ya kutokuamini kwao." Sivyo? Kazi nyingi kuu Yeye hawezi kutenda leo, kwa sababu ya kutokuamini.

240 Sasa, ni nani ambaye angeweza kutabiri *hilo*? Mungu. Ni nani yule ambaye alisema *hilo?* Mungu. Ni nani ambaye alitenda *hili?* Mungu. Ni nani ambaye alisema ambako yule dubu, paa, kulungu, mambo haya mengine yote, wale saba... yote—mambo haya yote ambayo yametukia? Ni nani aliyesema hayo? Yeye, Kristo, aliye ndani yetu, akitabiri Mwenyewe kupitia kwetu, akijifunua Mwenyewe kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Ni nani aliyetuliza zile pepo? Ni nani aliyeumba wale kindi? Yeye yule aliyeumba kondoo dume kwa ajili ya Ibrahim, wakati...alimwita Yeye "Yehova—yire." Hayo majina ya pamoja ya ukombozi yangali yanamhusu Yeye. Yeye bado ni Yehova-yire, "Bwana anaweza kujipatia Mwenyewe Sadaka."

241 Sasa, kila mmoja wenu, na—nataka unyofu wenu wa dhati sasa. Kama kwa kweli mtaamini kwa mioyo yenu yote, hakutakuwa na mtu mnyonge katikati yetu, ifikapo wakati saa ile itafikia dakika tano zaidi. Hapatakuwa na mtu hapa isipokuwa watakaokuwa wanatembea kwa miguu yao, wazima, kama tu mtaliamini. Mnaweza kuamini?

242 Sasa hebu tu tuone sasa kama Yeye atakuja kwetu na kujifunua Mwenyewe, tunapoinamisha vichwa vyetu.

243 Bwana Yesu, sasa Wewe unisaidie. Nami nitakutii Wewe, Bwana, kwa yote nijuayo. Nisamehe dhambi zangu na makosa. Naomba hilo katika Jina la Yesu. Amina.

244 Sasa hebu tuchukue upande huu hapa, mtu ye yote hapa. Amini, uwe na imani, usitie shaka! Mtu ye yote asiyenijua mimi, ikiwezekana. Siwezi kusema ono linaelekea wapi. Yanibidi niliangalie Hilo tu. Na kama Hilo likifanya hivyo, basi unajua, kama ni kweli au la. Wewe amini tu, na usitie shaka. Kama Yeye atalitenda, utaamini, unaona, baada ya yote haya ambayo yametendeka leo? Unaona? Hebu kubali tu kuponywa kwako, unaona. Sema, "Bwana, sasa ninamgusa Yesu Kristo. Ninaamini." Sasa Mungu wa Mbinguni na ajalie jambo hili.

245 "Yeye aliye ndani yako ni mkuu, Kristo, kuliko yeye aliye katika dunia." Sasa, katika mkutano, ambapo tunamgusa Yeye, Yeye hujionyesha Mwenyewe; kama yule mwanamke aliyemgusa Mungu, kupitia Kristo, na kuonyesha mahitaji yake.

246 Ninaona sasa huku kwenye kona hii, inaonekana kama ni mwanamume, ni mahututi sana. La, siyo. Ni mwanamke anamwombea mwanamume, na mwanamume huyo hayupo hapa. Lakini ni mwanamke. Ninaona kwamba mwanamke huyo . . . Ni ba—babaye, naye anakufa kwa kansa. [Ndugu Branham anatulia kidogo—Mh.] Na ni mahututi sana. Mtu huyo hayupo hapa. Yuko mahali pengine. Si nchi hii, hata. Ni, yuko Georgia. [Ndugu Branham anatulia.]

Endeleeni kuomba. Mnaamini kwa mioyo yenu yote sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina"—Mh.] Endeleeni tu kuomba, unaona.

Jina la mwanamke yule, anaomba, ni Bibi Jordan. Hatoki Georgia. Anatoka Carolina ya Kaskazini. Kama hilo ni kweli, bibi, simama kwa miguu yako. Sawa, yote ni kweli. [Yule dada anasema, "Asante Mungu! Asante Mungu!"—Mh.] Ulikuwa unaombea jambo hilo? ["Ndiyo, bwana; baba yangu."] Sawa. Sawa. [Yule dada anaendelea kuelezea habari za baba yake.]

Unaamini, kwamba, "Yeye aliye ndani yako ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia"? [Yule dada anasema, "Ninaamini."—Mh.] Unaamini kwamba Yeye aliye . . .

247 Angalia, hapa kuna jambo jingine. Umekuwa na mafunzo makubwa katika siku zako za mwanzoni, au jambo fulani, kwa sababu yaonekana kama umechanganyikiwa au katika namna fulani ya Mkristo . . . Je! baba yako si mhudumu, au mtu kama huyo, baadhi ya watu wako, au jambo fulani? [Yule dada anasema, "Mume wangu."—Mh.] Mumeo, huyo ndiye. Niliweza kuona mtu fulani akisimama karibu nawe, akihubiri Injili, nawe ulikuwa kanisani. Yeye alihusiana nawe. ["Bwana asifiwe!"] Naam, ndivyo hivyo.

Sasa, huyu bibi simjui, bali Mungu anamjua huyu mwanamke.

248 Sasa, una kitu cho chote kwenye pochi yako, leso ndogo au kitu fulani mle? Sawa, basi una pa- . . . Utakapoketi chini, weka mikono yako juu ya leso hiyo, nawe usitie shaka, na Yeye

aliye ndani yako ni mkuu kuliko yeye ambaye anamuua baba yako. Amini kwa moyo wako wote, hivyo itakuwa kama vile unavyoamini.

249 Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Simjui mwanamke yule. Kadiri nijuavyo, hiyo ni mara ya kwanza, nadhani, nimewahi kumwona. Lakini yuaketi pale katika hali ya kukata tamaa, akiomba. Na Mungu yeye yule hasa ambaye aliweza kugeuka na kumwambia mwanamke yule kuhusu kutokwa kwake na damu, ni Mungu yeye yule aliyepo hapa, akionyesha kwamba Yeye aliye ndani yako ameushinda ulimwengu. Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kama ukiwa tu na imani, usitie shaka.

250 Tukinena kuhusu kansa, ninaona kivuli kile cheusi tena. Kiko juu ya mwanamke, anayeketi papa *hapa*. Ana kansa ya koo, naye yuko taabani. Naye amekwisha kuombewa, na anajaribu kukubali kuponywa kwake. Bibi Burton, kama utaamini! Simjui mwanamke mwenyewe. Lakini kama utaamini kwa moyo wako wote . . . Kwa kweli, kitu hicho . . .

Hebu nikueleze jambo hili, unalojaribu kufanya. Umepwelewa na sauti, kutokana na jambo hilo, na unajaribu kuomba ili sauti yako irudi. Sivyo? Punga mkono wako *hivi*. Sasa, huyu mwanamke ni mgeni kwangu. Simjui. Mnamwona? Hiyo ni kweli. Ndiyo, huyo hapo. Unaona? "Yeye aliye ndani yako ni mkuu, imani ambayo inaweza kumgusa Yeye, kuliko yeye aliye kwenye koo lako."

Mnaamini kwa mioyo yenu yote? [Kusanyiko linasema, "Amina"—Mh.]

251 Dada Larsen, ninakufahamu. Yeye ndiye amenipangisha nyumba. Lakini, Dada Larsen, umeshamwona daktari au jambo fulani, kitu kama hicho. Unangojea kupasuliwa. Hiyo ni kweli. Sivyo? Yeye aliye ndani yako ni mkuu, Dada Larsen, kuliko yeye aliye katika dunia. Yesu alisema, "Nilikuwa mgeni, nawe ukanikaribisha Mimi. Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo sana, watoto Wangu, mlinitendea Mimi."

Ee Baba wa Mbinguni, uturehemu!

252 Waonaje? Unangojea kupasuliwa, pia. U mgeni kwangu. Sivyo? [Yule dada anasema, "Ndiyo."—Mh.] Wewe si mwenyeji wa hapa. ["Ninakujua, lakini wewe hunijui."] Wanijua, lakini mimi sikujui. ["Hunijui mimi."] Lakini Mungu anakujua. Unaamini hivyo? ["Ndiyo, ninaamini."] Unangojea kupasuliwa. Huishi hapa. Uko karibu na Bedford, Springville, kitu kama hicho . . . Ni mahali hapo, Springville. Bibi Burton . . . La, la, samahani, sikumaanisha hilo. Bibi Parker, hilo ndilo jina lako. Sivyo? Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko yeye anayejaribu kukuua. Sivyo? Unaamini kwa moyo wako wote? Basi hutahitaji kupasuliwa, kama unaamini.

253 Unafikiria nini kuhusu yote haya, dada? Mimi sikujui. Wewe u mgeni kwangu. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? [Yule dada anasema, "Ninaamini."—Mh.] Unaamini. Asante. Mungu ataheshimu jambo hilo. Wewe ni Bibi White. Unatoka Fort Worth, Texas. Una ugonjwa wa misuli, ugonjwa wa neva. U mahututi. Hakuna matumaini kwako, kulingana na sayansi ya madawa. Mumeo, ana haja ya kiroho ambayo anaiombea. Una mwanao hapo, yeye anaumwa na mgongo wake, na ugonjwa wa moyo. Una mvulana mdogo pajani mwake. Mvulana huyo mchanga ana namna fulani ya usemi ambao unaombea. Kama hilo ni kweli, inua mkono wako juu. [Mume anasema, "Hilo ni kweli. Ndiyo mahitaji yetu."]

"Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia." Mnaamini hivyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kwa mioyo yenu yote? ["Amina."] Kwa wote? ["Amina."]

Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu.

254 Sasa Yeye amepita kwenye jengo. Amewathibitishia kwamba Yeye ni Mungu. "Ni mkuu zaidi, Huyu aliye ndani yenu, kuliko yeye aliye katika dunia." Ni Bwana Mungu. Sasa, Yeye aliye ndani yenu, mwache Yeye apate nafasi ya kwanza. Mwache Yeye awe na sauti ya kwanza ya—ya yale wewe . . .

Sema moyoni mwako sasa hivi, kama ukiweza, kwa moyo wako wote, na uamini, "Ugonjwa ambao ulikuwa mwilini mwangu umekwisha." Unaona? "Siumwi tena. Sina ugonjwa tena. Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye mwilini mwangu. Yeye aliye moyoni mwangu ni mkuu kuliko yeye aliye mwilini mwangu. Kwa hiyo, Yeye aliye moyoni mwangu aliziumba Mbingu na nchi. Mwili wangu umechafuliwa na Shetani, nami ni hekalu ambamo anaishi Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, Shetani, nakuamuru kuuacha mwili wangu. Katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani yangu." Unaona? Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Sasa wote na tuombe jinsi tutakavyo sasa, kila mmoja, ninapowaombea.

255 Mungu Mwenyezi, Muumba Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa uzima, Mfunuaji wa siri za mioyo, Wewe ulisema, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na hata hutambua mawazo ya akili."

256 Hiyo ndiyo sababu, wakati Neno lilipofanyika mwili, lilijua ambalo walikuwa wanafikiria, wakati Yeye alipoyatambua mawazo yao. Yeye alikuwa Neno, na Neno lilijua siri za mioyo yao.

Na Neno hilo bado ni Neno lile lile. Na usiku wa leo tunaliona Hilo likujifunua Lenyewe ndani yetu, baada ya miaka elfu mbili, kwa sababu Yeye aliliandika kwenye karatasi na yuko hapa akilithibitisha, akionyesha, kwamba ni sahihi.

257 Hapa pana leso zimewekwa hapa. Wagonjwa wapo kila mahali. Ninaomba kwamba Roho Mtakatifu mkuu aliyepo, ambaye huonyesha mambo haya, ambaye hunena mambo haya, na kamwe hashindwi, ila lililo sahihi, hawezi kushindwa hata wakati mmoja, kwa sababu Huyo ni Mungu. Na apake mafuta leso hizi kwa Uwepo Wake, na kuponya kila mgonjwa atakayewekelewa. Na Mungu Ambaye anaweza kuishi, baada ya miaka elfu mbili, na anaweza kujifanya Mwenyewe ndani ya mioyo ya wenye dhambi ambao wamekombolewa kwa neema na imani, na aweza kunena Maneno Yake Mwenyewe kupitia midomo ipatikanayo na mauti, na tuone ikitokea sawa kabisa na yale aliyoahidi.

258 Ee Bwana Mungu, nakuomba uturehemu. Na jalia kila mwanamume na mwanamke ambaye ameketi sasa, ambaye ana namna yo yote ya maradhi au mateso; na kama vile Musa alivyojitupa mwenyewe katika pengo, kwa ajili ya watu, usiku wa leo ninaweka moyo wangu mbele Zako, Bwana. Na kwa imani yote niliyo nayo, ambayo iko ndani Yako, ambayo Wewe umenipa, ninawapa. Kama Petro alivyosema penye mlango uitwao Mzuri, "Nilicho nacho, ndicho nikupacho. Kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende." Na mtu yule alikuwa kilema na—na mnyonge kwa muda mfupi, lakini, walipokuwa wamemshika, mifupa ya vifundo vya miguu ikatiwa nguvu. Naye akaingia katika Nyumba ya Mungu, akirukaruka, na akimsifu na kumbariki Mungu.

259 Wewe u yeye yule jana, leo, na hata milele. Na mitume Wake wakasema, "Nilicho nacho, ndicho nikupacho." Ilikuwa imani. Nami ninasema: nilicho nacho, nawapa wasikizi hawa! Kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, kataeni magonjwa yenu, kwa sababu Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko huyo Ibilisi anayejaribu kuyatwaa maisha yenu. Ninyi ni wana wa Mungu. Mmekombolewa.

260 Ninaamuru kwamba Shetani awaache watu hawa. Mungu aliyeondoa tufani ile hapa juzijuzi, Mungu aliyetuliza pepo na dhoruba, Yeye na ahakikishe ya kwamba kila ugonjwa umeondolewa kwa watu hawa, na nguvu za Kristo zimedhihirishwa katika maisha yao saa hii. Kila mwenye dhambi na atubu. Na kila mtu, asiyekuwa karibu na Wewe, afanye hivyo sasa hivi. Na iwe hivyo, katika Jina la Yesu Kristo.

261 Nami, kama mchungaji wenu, ndugu yenu, kwa imani niliyo nayo, nimemwomba Mungu aiweke hiyo juu yenu. Ninaamini kwamba nitapokea kile nilichoomba. Sasa ikiwa mtaamini pamoja nami; kwa imani ile niliyo nayo, ninawapa hiyo sasa hivi.

Na sasa, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kataeni mateso yenu, magonjwa yenu, na mseme "Huna budi kuondoka," sababu mnayo imani yenu, na imani yangu, pamoja na nguvu za Yesu Kristo, Ambaye uwepo Wake wa kila mahali

upo hapa kudhihirisha jambo hilo na kuthibitisha kwamba Yuko hapa, atawapa afya sasa.

262 Je! Waamini hilo, bibi, uliyelala kwenye machela haya? [Yule Dada anasema, "Hiyo ni kweli."—Mh.] Hata misuli yako ikiwa kama vile wasemavyo, mishipa imeshupaa na kadhalika, waweza kutembea kama utajaribu. Simama, katika Jina la Yesu Kristo. Msaidieni pale. Huyo hapa anatembea. Je! hamuamini? Wengine wote, simameni. Mifupa ya vifundo vyake vya miguu, imepata nguvu.

Sasa hebu na tuinue mikono yetu na tumsifu Yeye.

263 Yehova Mkuu Aliye Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, twajikabidhi Kwako kwa ajili ya kuponywa. Amina.

Yeye Aliye Ndani Yenu SWA63-1110E
(He That Is In You)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni Novemba 10, 1963, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1991 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org